# *KAMA TAI ATAHARIKISHAVYO KIOTA CHAKE*

(Ni sawa. Vema. Ni sawa.)

Mambo yote yanawezekana, Bwana, naamini.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

2 Bwana mwenye rehema, tunakikaribia kiti Chako cha rehema katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Tunataka kukushukuru kwa baraka zote ambazo umetukirimia. Jinsi ambavyo umekuwa mwema kwetu! Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utaendelea kuwa pamoja nasi.

3 Wengi ni wagonjwa na wahitaji, nasi tunaomba ya kwamba nguvu Zako zitawaponya. Nina furaha sana kuchukua barua hizi, taarifa kutoka kwa watu ambao wamekuwa hapa ambao wakati mmoja walikuwa wagonjwa, wakiteseka, na hata wakatangazwa na madaktari, wamepona sasa. Mungu, jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu, mwishoni mwa ibada.

4 Neema ya Mungu na iwe pamoja nasi. Wale wanaokuja na kuutafuta wokovu, Ee Mungu, jalia waupate Mwamba huo katika nchi yenye uchovu, Kimbilio wakati wa dhoruba. Pia jalia Roho Mtakatifu mkuu, Bwana, ambatize kila mwaminio katika Mwili wa Kristo, kwa Uwepo Wake na ubatizo wa utu Wake.

5 Wakumbuke wale wanaopata ahueni, Bwana, hivi kwamba hawawezi kusogezwa, kulazwa hospitalini, na vinginevyo. Tunaomba, Baba, ya kwamba Roho Wako atawaponya.

6 Sasa, jalia Roho Mtakatifu achunguze kila moyo ulio humu ndani usiku wa leo. Jalia huu uwe ni wakati wa kutafuta, jalia uwe wakati wa uaminifu na kujichunguza. Tunaomba ya kwamba utalibariki Neno tunapolisoma. Halafu basi, Roho Mtakatifu na achukue kila kitu kinachohitajika hapa usiku wa leo, akiliweka Neno moja kwa moja juu yake kusudi tuweze kuona ya kwamba tuna baraka ya ukombozi inayongoja. Tujalie, Baba, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

7 Ketini. Hakika tumekuwa na siku nzuri sana leo. Nilikaa muda mrefu kidogo jana usiku mkutanoni, m—mke na wengineo karibu hawakuweza kunizindua kwa yapata dakika kumi baada ya kuondoka humu jengoni, ni kwamba kidogo nilikaa mstarini muda mrefu kupita kiasi, nafikiri.

8 Si wakati unapokuwa *huko* juu, mnaona, huko juu katika ule upako mtukufu, wala si wakati ukiwa hapa chini, la muhimu ni katikati, wakati ukitoka nahali pamoja hadi pengine, ukishuka

kutoka kwenye upako huo kurudi kwenye huu tena. Lakini inakwambia nini? Kuna Nchi ng'ambo ya mto, naam, kuna Mahali halisi ambapo tunaweza kupata amani, na furaha, na utoshelevu.

9 Na sasa, Bwana akipenda, kesho usiku tutagawa kadi za maombi saa kumi na mbili na nusu, hao wavulana watazigawa. Na kisha, wala hatuna wakati mwingi zaidi, sivyo? Tuna kesho tu usiku ambayo itakuwa Ijumaa, sivyo? Ijumaa, Jumamosi, na Jumapili, siku tatu zaidi usiku. Vema, hiyo ni . . .

10 Kila mtu anayetaka kuombewa, na kadhalika, ingieni sasa hivi mchukue kadi zenu za maombi, nasi tutawaita moja kwa moja mstarini, na kuwaombea, na kufanya kila tuwezalo. Na ikikubidi kuondoka kabla ibada haijaisha, nenda kwenye chumba cha dharura, nasi tungeitaka Hiyo ije hapa nje, ndipo Roho Mtakatifu anaweza kuona kama kuna kitu fulani maishani, wakati ikiwa chini ya upambanuzi huo.

11 Unaona, kama una jambo ambalo umefanya, ama jambo ambalo hujafanya, jambo ulilopaswa kufanya, unaona, haidhuru utaombewa kiasi gani, kamwe hautakuacha mpaka jambo hilo litakapowekwa sawa. Ungeweza tu kutetemeka, kuwekewa mikono, na kumwagiwa mafuta, hautaondoka, utakaa papo hapo.

12 Angalieni, kulikuwa na . . . Yesu aliwapa wanafunzi Wake nguvu za kutoa pepo. Ni wangapi wanaojua hilo? Hakika. Siku kumi baadaye tunawaona wote wameshindwa na ugonjwa mmoja wa kifafa. Mnaona? Lakini wakati . . . Huyo ibilisi alilala pale pale. Ndipo basi Yesu alipokuja, basi huyo ibilisi alijua ya kwamba alikutana na Kitu fulani hilo lilikuwa katika kiwango cha juu zaidi kuliko kile walichokuwa nacho hao wanafunzi, ndipo ikambidi kutoka.

13 Sasa, lazima daima tuje tumeomba kabisa, tumeungama kabisa, na tayari kuponywa. Ndipo ukifanya hivyo, kuna kitu kimoja tu kilichosalia, kumtupa huyo adui nje, hivyo tu. Kama umeomba kabisa, nawe una hakika ya kwamba ni mapenzi ya Mungu kukuponya, nawe umeomba kabisa juu yake, hilo—hilo latosha, unaona. Kuna jambo moja tu la kufanya basi, jambo pekee karama inaloweza kufanya ni kumtoa, yote yamekwisha. Mnaona? Imekwisha basi. Nami nina furaha sana kwamba tunaweza—tunaweza kujua, tunajua jambo fulani limetukia wakati—wakati linapotukia.

14 Leo ilikuwa . . . Asubuhi ya leo, mapema, niliamka, wala sikulala vizuri sana jana jioni, nami nikaamka mapema asubuhi ya leo, naye Roho Mtakatifu alikuwa akizungumza nami, Naye akaniambia, "Toka, nitakutumia."

15 Na kwa hiyo, jambo pekee ninalojua kufanya ni kutoka tu, hivyo tu. Nami nikawazia, "Vema, gari langu linahitaji kubadilishwa grisi, kwa hiyo nitaninii tu, ama mafuta, hasa,"

kwa hiyo nikaenda kwenye kituo cha mafuta. Nikawaza, "Bwana, labda ni baadhi ya jamaa hawa hapa." Ndipo nikazungumza na mvulana mzuri Mpresbiteri, akisafirisha petroli, na zinginezo, ilionekana kana kwamba si jambo la dharura.

16 Ndipo ajali ikatokea kwenye kona, nikasema, "Hii hapa." Nikatoka nikaenda pale, lakini hakuna mtu aliyeumia, kwa hiyo wao. . .halikuwa hilo, kwa hiyo nikaingia kwenye gari langu, nikawaza, "Nitarudi nyumbani."

Nikaanza kushuka kwenda nyumbani, na vema, Kitu fulani kikasema, "Endelea tu kuendesha gari."

17 Kwa hiyo nimekuwa nikiandaa viwanja vyangu vya maombi huko juu karibu na Mlima Rainier, hapa juu, nikirudi kichakani. Na kuna jambo fulani kuhusu kwenda mahali yalipo maumbile, unamwona Mungu, kaa—kaa tu peke yako. Nami nilikuwa na mtoto Joseph pamoja nami, mvulana wangu mdogo, ndipo Kitu fulani kikasema, "Nenda kando ya barabara hapa na usimame, kwa sababu ni ninii. . .angalia, acha huyo mvulana mdogo amtazame huyo mvuvi."

18 Vema, walivua samaki kama dakika kumi, wakaondoka, kwa hiyo mimi na Joseph tulikuwa tumeketi pale. Vema, nikawaza, "Vema, tutaenda basi kwenye uwanja wa maombi, kisha nitamwacha Joseph acheze huku nikisoma na kuomba, kisha tutashuka turudi." Mimi hula, yapata, mara moja kwa siku.

19 Kwa hiyo, Kitu fulani kisingeniacha niondoke. Ndipo nikawazia, "Vema, Joseph, nina zulia chini ya kiti, hebu tuoshe tu mi—mikeka kwenye gari la kanisa." Ninaendesha gari lao, kwa hiyo nikawazia ningeninii tu, ningetaka kulishughulikia. Nami, nikiosha mikeka ya sakafuni, nami nikawazia, "Hilo ni sawa."

20 Nami nilikuwa nimefungua mlango, Joseph, alikuwa akifanya yake kwenye gurudumu pale chini, mwajua, maskini jamaa huyo kidogo akijiburudisha. Ndipo ghafla, gari likasimama, likaanza kurudi nyuma, mtu fulani alifikiri kwamba mtu fulani alikuwa na haja. Ndipo basi, nilipopata kujua, katika gari hili kulikuwa na mwanamke akifa kwa kansa, mke wa mhudumu. Nao walikuwa wameongozwa kiajabu sana, walikuwa wameenda mahali ninapokaa, nami nilikuwa nimeondoka. Wakaacha leso ipate kuombewa, kisha wakapitia njia nyingine waliyopaswa kupitia, ndipo Kitu fulani kikawaambia, "Geukeni mrudi nyuma."

21 Nao wakazunguka upande huu mwingine, walikuwa wakishuka, kasema, "Si ni ajabu hii kwa nini tungekuwa tukipitia huku?" Na papo hapo, kasema, "Sijui kama hao watu wana shida, mle kwenye gari?"

22 Wakati uo huo, nilikuwa ndani ya gari, nimeinamisha kichwa chini, nikisugua huku na huku, namna hiyo. Nami nilikuwa niondoke, katika dakika zingine chache nilikuwa nikisogea kwenye mahali pa maombi, na huyo hapo mwanamke amelala nyuma ya gari, akifa kwa kansa. Jinsi Mungu alivyoimwaga Roho Yake mle ndani!

23 Si ni ajabu jinsi anavyofanya kazi? Jinsi atakavyotuongoza kwa njia ya ajabu mahali mahali, kufanya tu kila kona kukutana kama tu. . .! Ni. . .Hilo si bahati tu, hilo limeongozwa kiroho. Mnaamini hilo, sivyo? Wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu.

24 Sasa hebu na tufungue Maandiko usiku wa leo, kwa ajili ya somo la Maandiko, katika Kitabu cha Kumbukumbu la Torati, mlango wa 32, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 7, na tusome sehemu moja sasa, mpaka kifungu cha 12 pamoja:

> *Kumbuka. . .za kale. . .Kumbuka siku za kale, tafakari miaka ya vizazi vingi: mwulize baba yako, naye atakuonyesha; wazee wako, nao watakuambia.*
>
> *Yeye Aliye Juu alipowapa. . .mataifa urithi wao, alipowabagua wanadamu, aliweka mipaka ya hao watu, kwa kadiri ya hesabu ya wana wa Israeli.*
>
> *Maana sehemu ya BWANA ni watu wake; Yakobo ni kura ya urithi wake.*
>
> *Alimkuta katika nchi ya ukame, na. . .jangwa tupu, litishalo; alimwongoza kote, akamfunza, akamhifadhi kama mboni ya jicho lake.*
>
> Na *mfano wa tai ataharikishaye kiota chake, na kupapatika juu ya makinda yake, alikunjua mbawa zake, akawatwaa, akawachukua juu ya mbawa zake:*
>
> *Basi BWANA peke yake ndiye aliyemwongoza, wala hapakuwa na mungu mgeni pamoja naye.*

25 Ningetaka kuchukua somo, ambalo kama ni mapenzi ya Bwana usiku wa leo, la kipekee, la kigeni, lakini: *Kama Tai Atarikishavyo Kiota Chake, Apapatikavyo Juu Ya Makinda Yake, Akawachukua Juu Ya Mbawa Zake, Na Kuwapeleka Juu.*

26 Mara nyingi nimeshangaa ni kwa nini Mungu aliwahi kulinganisha urithi Wake na tai. Ndipo siku moja nikaona katika Biblia ya kwamba Mungu hujiita Mwenyewe Tai, Yeye ni Yehova-Tai, na watoto Wake ni makinda wa tai, watoto wa tai chini ya mbawa za Yehova.

27 Na kama mwanamaumbile, ni—ninapenda kuchunguza maumbile. Biblia yangu ya kwanza ilikuwa ni maumbile, jinsi nilivyoona jinsi, kila kitu kikitendeka katika maumbile, na jinsi ilivyobidi iwe ni Mungu, hakuna kitu kingine kingaliweza kuwa hivyo ila Mungu. Ndipo likaniongoza kuamini ya

kwamba kulikuwako na Nguvu fulani kuu sana mahali fulani, zilizoyadhibiti mambo haya yote. Kama vile sisi . . .

28 Huko India, si muda mrefu uliopita, nilikaribishwa na dini kumi na saba mbalimbali alasiri moja katika hekalu la Jaini, walikuwa na Budha, Waislamu, Makalasinga, Wajaini, na kadhalika, nao ni—wao ni watu wa kipekee sana. Lakini kati ya dini hizi zote kumi na saba, karibu zote, mbali na Waislamu na wengine wachache, wanaamini katika kuzaliwa tena katika mwili mwingine.

29 Hata, walibeba ufagio mdogo, nao wangeifagia sakafu, kusudi tu wawe na hakika, wanapotembea, wasimkanyage nzi mdogo wala mdudu, kwa sababu huenda akawa ni mjomba wao, au shangazi, ama mtu fulani ambaye amerudi. Ungewezaje kamwe kuhubiri dini ya damu kwa watu ambao hawangeua nzi. Mnaona? Na kwa hiyo, ilinibidi tu kungojea, kumwacha Mungu afanye hivyo Mwenyewe, lakini bila shaka alifanya jambo kubwa sana huko India.

30 Lakini tukiangalia maumbile na kuona jinsi ambavyo kila kitu hufanya kazi, basi utajua ya kwamba hapo, msingi wa Ukristo. Na Ukristo ndiyo dini pekee iliyo sahihi, kwa sababu Ukristo umewekewa msingi juu ya mauti, kuzikwa, kufufuka.

31 Sasa, si ubadilishaji. Sasa, kama nikiangusha karatasi hii sakafuni, na kusema, "Vema, niliangusha *hiyo*, nitairudisha *hii* mahali pake," huo sio *ufufuo*, huo ni *ubadilishaji*. Bali Yesu yeye yule aliyeingia ardhini, Yesu yeye yule alirudi kutoka ardhini. Basi ufufuo, ama, Ukristo umewekewa msingi juu ya ufufuo. Kwa hiyo, unapoweza kuona misitu, na miti, na kuangalia . . .

32 Hapa miezi michache, vema, ni yapata mwaka huu ujao, yapata majuma manne, matatu tangu sasa, nilikuwa huko chini Kentucky nikiwinda kuchakulo. Nasi tulikuwa na mkutano karibu sana, yapata miaka miwili kabla ya hapo, kwenye uwanja wa kambi wa Kimethodisti, kwa siku mbili usiku. Bwana alifanya mambo makuu—makuu miongoni mwa Wamethodisti.

33 Na kwa hiyo, hao, Wamethodisti walikuwa wanaamini katika uponyaji wa Kiungu. John Wesley aliamini, nina kitabu chake, kitabu chake cha kiada, na kadhalika, muhtasari wake. Na kwa hiyo, yeye . . . Walikuwa wanaamini katika uponyaji wa Kiungu, wengi wao bado wanaumini.

34 Na kwa hiyo, kulikuwako na uamsho mkuu miongoni mwa hao watu. Kwa hiyo, uwanja huu mkubwa wa kambi kule chini, huko chini katika Methodisti ya kusini, walikuwa wamenialika kule chini kwa ajili ya u—uamsho, nami nilikuwa nimetumia Jumamosi na Jumapili pamoja nao.

35 Naye Bw. Wood, ambaye hapo awali alikuwa ni Shahidi wa Yehova, na mvulana wake kiwete, mguu wake umepindika nyuma chini yake, kijana, ameketi huko nyuma mkutanoni, baba yake ameketi pale akikosoa, mama yake ameketi pale akiomba,

Roho Mtakatifu akageukia mahali ambapo kulikuwa na, nakisia, angalau watu elfu nane au kumi, na kusema, "Huyo jamaa mdogo aliyeketi hapo nyuma na mguu uliolemaa, baba yake ni Shahidi wa Yehova naye ni m—mkandarasi, jina lake ni Banks Wood, mama yake ni Mmethodisti. Jina la mvulana huyo mdogo ni David, BWANA ASEMA HIVI, simama kwa miguu yako, Yesu Kristo anakuponya." Huyo akasimama; hata hajui ulikuwa ni mguu gani sasa, isipokuwa alitokea . . .

36 Kwa hiyo, Bw. Wood, akaokoka kwelikweli, naye akaingiza jamaa yake yote ndani, baba yake, na mama yake, na hao wote, ndani ya agano la Kristo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

37 Basi mimi na na yeye tulikuwa tukiwinda, tulikuwa tumeshuka yapata majuma mawili, naye akasema . . . Kulikuwa kukavu sana, ilitubidi kushuka sehemu za chini kutafuta mahali palipokuwa na unyevu wa kutosha kutembea, la sivyo hao kuchakulo wangekusikia. Na kwa hiyo, akasema, "Ninajua mahali palipo na mtu aliye na ekari mia tano, lakini," kasema, "nina shaka sana kwamba ataniruhusu kuwinda, kwa sababu yeye ni kafiri kindakindaki."

Nami nikasema, "Huyo angekuwa jamaa mzuri kwetu kukutana naye."

38 Kwa hiyo tukaenda kule, naye akasogea mbele ya nyumba yake, naye alikuwa ameketi barazani, akizungumza na mzee mmoja, basi tulipokuja, Bw. Wood alitoka na kulizunguka gari, naye akasema, "Halo, Jim," ama lolote lililokuwa jina lake.

Kasema, "U hali gani?"

Akasema, "Sidhani unanijua."

Akasema, "Naam, ninakujua. Ninaamini wewe ni mvulana wa Jim Wood."

Akasema, "Hiyo ni kweli."

39 Akasema, "Sijui kama ningeweza kuwinda hapa nyuma?" Kasema, "Ni kukavu sana, tumekuwa tukiwinda kwenye kijito kingine, kiitwacho Dutton," kisha kasema, "ni kukavu sana huko."

40 Akasema, "Nina ekari mia tano hapa, mwana yeyote wa Jim Wood anaweza kufurahia popote anapotaka au wakati wowote anaotaka." Kasema, "Kamwe sijapata kuwa na rafiki mwaminifu maishani mwangu kuliko Jim Wood."

Akasema, "Asante." Akasema, "Sasa, nimeambatana na mchungaji wangu."

Akasema, "Wood, humaanishi kusema umekuwa duni sana, mpaka inakubidi kubebana na mhubiri popote uendapo?"

Naye akasema, "Vema, sijui kuhusu hilo, lakini mimi . . . "

Ndipo nikashuka kwenye gari, na nikasogea karibu, na kusema, "U hali gani, bwana?"

Akasema, "U hali gani?" Vema, akasema, "Nawe ni mhubiri ati?"

Damu ya kuchakulo, na uchafu, loo, jamani, masharubu yapata urefu *huo*, nikasema, "Naam, bwana, nadhani ndivyo nilivyo."

Naye akasema, "Vema, nadhani Wood amekwambia ya kwamba mimi ni kafiri?"

Nikasema, "Vema, alisema jambo fulani kulihusu, lakini sidhani kama mtu anayeonyesha wema ulio nao angekuwa kweli ni kafiri." Nikasema . . .

Akasema, "Vema, ninadhaniwa kuwa."

Nikasema, "Nina furaha umesema *unadhaniwa* kuwa."

41 Naye akasema, "Vema," akasema, "Hebu nikwambie," kasema, "Sijapata kuona chochote ambacho kingeweza, zaidi ya saikolojia tu, kingeweza kamwe kunithibitishia ya kwamba kuna chochote cha Mungu." Akasema, "Ninawasikia wahubiri hawa wakipiga makelele na kuzungumza kuhusu kulikuwako na Mungu," kisha kasema, "Alikufa huko nyuma muda mrefu uliopita, miaka elfu mbili iliyopita." Halafu kasema, "Mungu kama huyo angenifaa nini ambaye amekufa miaka elfu mbili iliyopita, nikisha kufa?" Mnaona?

Nikasema, "Naam, kama hilo lililimalizia, hakika uko sahihi." Nikasema, "Hilo halikulimalizia."

Naye akasema, "Vema, kuna . . . Sijaenda kanisani," akasema, "kwa karibu miaka hamsini." Alikuwa na umri wa kama miaka sabini na mitano.

Nikasema, "Hilo si jambo la kujivunia sana, sivyo, bwana?"

42 Akasema, "La, nafikiri si la kujivunia." Akasema, "Lakini kuna mhubiri aliyekuwa na mkutano hapa nje kwenye," akasema, "hapa Acton si muda mrefu uliopita, kwenye uwanja huo wa kambi wa Kimethodisti." Akasema, "Kama jamaa huyo akiwahi kuja nchini tena, nitamsikiliza."

Nikasema, "Naam, bwana." Ndugu Wood aliniangalia na kukonyeza jicho, mwajua. Nami nikasema, "Naam, bwana." Nikasema, "Jina lake lilikuwa nani?"

43 Kasema, "Sijui jina lake." Akasema, "Lakini maskini Aunt Melissie *Nanii* aliishi hapa juu kilimani." Kasema, "Mimi, mimi na mke wangu, tulikuwa tukienda huko kwa majuma mawili, tukimsimamisha, na kuvuta shuka la kuchomoa, hata asingeweza kusogea kwa sababu ya kansa ya tumbo." Kisha kasema, "Madaktari walimkatia tamaa miezi kadhaa kabla ya hapo." Nao wakasema wao, ya kwamba asingeweza, hata wasingeweza kumweka kwenye maliwato ya kitandani.

44 Kisha kasema, "Dada yake alihudhuria mkutano huo usiku huo." Kasema, "Kulikuwa na yapata, labda, watu elfu tatu

huko nje kwenye uwanja wa kambi." Kisha kasema, "Mhubiri huyu, usiku wake wa kwanza pale, aliangalia nyuma kwenye kusanyiko hilo na kumwita mwanamke huyu kwa jina, na kumwambia alikuwa ni nani mwanamke huyu aliyekuwa akimwombea. Ndipo mwanamke huyo akaanza kulia, kasema, 'Sasa, chukua leso hiyo uliyoipangusia machozi, uende ukaiweke juu ya huyo mwanamke, kwa kuwa BWANA ASEMA HIVI, ataishi.'"

45 Kisha kasema, "Nilifikiri walikuwa na Jeshi la Wokovu kule juu kilimani, usiku huo, waliporudi kule, kule kupiga makelele na mayowe," kasema, "tulifikiri ya kwamba mwanamke huyo alikufa." Kisha kasema, "Mimi na mke wangu tukavaa nguo zetu, yapata saa nne usiku tukapanda kwenda kule, naye alikuwa anakaanga sambusa za matofaa na kuzila." Kisha kasema, "Hata asingeweza kunywa maji ya shayiri asubuhi hiyo." Akasema, "Na sasa yeye hafanyi kazi yake tu, yeye hufanya kazi za majirani wote."

Nami nikasema, "Hilo lilikuwa jambo zuri sana!"

Akasema, "Sasa, wakati mimi. . .jamaa huyo atakaporudi hapa chini tena, nitaenda kumsikiliza."

Nikasema, "Vema, nawe. . .Hilo lingekufanya umwamini Mungu kama ukiona kitu kama hicho?"

Kasema, "Vema," kasema, "sasa, na—nadhani hicho ni kitu unachoweza kuona."

46 Nikasema, "Vema, hilo lilikuwa sawa." Nikaokota tu tofaa dogo pale. Ni wangapi wanaojua nyigu ni nini? Na kwa hiyo, nyigu yuko kwenye tofaa hili, nikamfukuza, ndipo—ndipo nikaanza kula hilo tofaa. Nikasema, "Hayo ni matofaa mazuri."

Kasema, "Naam, ndivyo."

Nikasema, "Mti huo una umri gani?"

Akasema, "Vema," kasema, "niliupanda hapo." Kasema, "Nakisia mti huo una umri wa kama miaka thelathini na mitano, ama arobaini."

Nikasema, "Je, huzaa matofaa kila mwaka?"

Akasema, "Naam, hakika huzaa." Alidhani nilikuwa nikijaribu kubadilisha hiyo hoja, mnaona.

47 Kwa hiyo nikasema, "Vema, nataka kukuuliza jambo fulani." Nikasema, "Hii ni yapata katikati ya Agosti, ama, juma la mwisho la Agosti," nami nikasema, "niliona majani yanapukutika kutoka kwenye mti huo."

Naye akasema, "Ndiyo, naam."

Halafu nikasema, "Kwa nini. . .? Sijui ni kitu gani kingeyafanya hayo majani kupukutika kutoka kwenye mti huo."

Akasema, "Utomvu umeshuka chini."

Nikasema, "Kwani ulienda wapi?"

Kasema, "Ulishuka chini mizizini."

"Um-hum." Nikasema, "Vema, ni kitu gani kinachoufanya ushuke kule chini?"

Akasema, "Kwani unaelekea wapi?"

"Vema," nikasema, "hakika, kabla hapajakuwapo na jalidi yoyote ama chochote kile, ilibidi Kitu fulani kiuonye huo utomvu uingie chini mizizini."

Naye akasema, "Vema," akasema, "ni maumbile tu."

"Vema," nikasema, "hebu weka kopo la maji kwenye nguzo, uone kama yatashuka." Mnaona?

Naye akasema, "Vema, unamaanisha nini?

48 Nikasema, "Bwana, ungekubali ya kwamba kuna Kitu fulani kinachochukua utomvu huo kama ungekaa hapa juu, kingeua huo mti, kamwe hungepata tofaa lingine, kwa hiyo Kitu fulani kinauonya utomvu huo, nao unashuka chini mizizini mwa huu mti mpaka kwenye majira ya kuchipua na kujificha, kisha unapanda na kukuletea zao lingine la matofaa."

Kasema, "Hiyo ni kweli."

49 "Vema," nikasema, "akili ile ile iliyouambia mti huo, ule utomvu kwenye mti huo, 'Ingia chini mizizini, wakati wa baridi kali unakuja,' kabla hata hatujapata kipindi cha baridi au jalidi, 'shuka huko chini ukajifiche,' hiyo ndiyo Akili ile ile iliyoniambia ya kwamba mwanamke huyo ataishi."

Akasema, "Wewe si yule mhubiri!"

Nikasema, "Ni mimi." Haya basi . . . Mnaona?

Vema, akasema, "Unajua nini? Njoo hapa, ninataka kukupa mkono." Kasema, "Kamwe sikuwazia hilo."

Nikasema, "Bwana, Mungu yuko kote karibu nawe."

50 Ni nani anayeweza kufanya ua moja rangi moja, na lingine rangi nyingine, aina ile ile kwenye jua lile lile, kwenye lile lile . . . ona, kufanya moja la waridi, na lingine jekundu, na hilo lingine jeupe, na kadhalika? Mungu. Mungu yuko katika maumbile. Kama tu utamchunguza, Yeye—Yeye anaishi katika maumbile.

51 Nilipoanza kuona ya kwamba Mungu alijiita Mwenyewe Tai, na kuwaita watoto Wake, tai, manabii Wake, ndipo nikashangaa ni kwa nini. Basi nikaanza kusoma juu ya tai. Tai ni ndege mkubwa. Sasa, neno lenyewe *tai*, kuna aina arobaini mbalimbali za tai tunaowajua, *tai* linamaanisha "araruaye kwa mdomo."

52 Halafu basi, ta—tai ni ndege wa kigeni, anaweza kuruka juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote aliyepo, hakuna ndege mwingine anayeweza kumfuata tai. Kama mwewe angejaribu kumfuata tai huyo, angevunjika-vunjika hewani, hajaumbiwa hilo. Tai anaweza kupaa juu sana hivi kwamba hakuna

ndege mwingine anayeweza kumkaribia, anaweza kwenda hata asionekane tena, apande tu juu kabisa.

53 Vema sasa, haitamfaa kitu kupanda kule juu, isipokuwa amejengwa apate kubakia hai wakati akiwa huko juu. Na hiyo ndiyo sababu Mungu aliwaita manabii Wake tai. Kadiri unavyozidi kupaa juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Vema basi, kama hana jicho ambalo anaweza kuonea, jicho lake litalinganishwa na kupanda kwake, basi ingefaa nini, kupanda kule juu, kama alikuwa kipofu?

54 Kwa hiyo hivyo ndivyo watu wengi hujaribu kupanda juu sana, nao ni vipofu baada ya kufika kule, kwa hiyo kuna faida gani kupanda kule juu? Mnaona? Unafikiri utapata Ph.D. yako, L. maradufu D., D.D.D., Q.S.D., na digrii za—za kila aina. Lakini vipi kama ukifika kule huku hustahili? Ungekuwa kipofu kwa kitu kile kile ulichopanda juu yake, isingefaa chochote, huwezi kuona nyuma tena. Kama vile ndugu alivyosema kuhusu ufunguo hivi majuzi, aliondoka, ama, huyo mtu aliondoka.

55 Kwa hiyo tai, kusudi apande juu, hana budi kuwa ndege aliyeumbwa maalum; na mtu, kuwa mtumishi wa Bwana ni mtu maalum. Hana budi kubadilishwa kwa ndani, na kufanywa upya tena. Hiyo ndiyo sababu Mungu huwaita watoto Wake, manabii Wake tai, hana budi kupanda juu, jicho lake.

56 Na jambo lingine, kama huyo tai angejaribu kupanda juu kule akiwa na manyoya ya kawaida tu, kama yaliyo katika kunguru, ama kama katika—katika njiwa, mbona, kila unyoya ungemtoka. Uliwahi kujaribu kung'oa unyoya kutoka kwa tai? Afadhali uchukue koleo na kumkanyaga kwa miguu, kwa sababu hayo manyoya kweli hudumu pale. Kama hayakudumu, yeye, ingemwangusha tai wakati atakapofika kule juu kwenye zile milki ambamo ndege wengine, kwa hiyo mnaona, hana budi kuwa ndege maalum.

57 Jambo lingine kuhusu tai, tai ni nde—ndege maalum, kwa sababu kamwe hatajenga kiota chake ardhini, yeye hujenga kiota chake juu *kabisa*. Analinganisha hilo na Kanisa Lake, "Ninyi ni mji ulio juu ya kilima," si katika bonde. "Ninyi ni mji ulio juu ya kilima, unaoweza kuonekana kwa mbali. Mshumaa uliowashwa, unaweza kuonekana mbali sana." Kanisa likiwa juu, likiwa na matarajio makubwa, malengo makuu.

58 Sina matumaini mengi kwa kanisa la mchungaji ambaye hana malengo ya wao kujiboresha siku baada ya siku, na mwaka baada ya mwaka. Kanisa ambalo kweli ni kanisa la Mungu aliye hai kamwe halitakoma, kusema, "Vema, ndiyo kwanza niingie, nadhani ni sawa sasa." Hilo si Kanisa la Mungu, yeye ana shauku ya kusonga mbele.

"Vema, nilitekeleza sehemu yangu, nilimleta mwenye dhambi mmoja mwaka huu, naye akaokoka."

59 Ndugu, hiyo siyo shauku ya Kanisa la Mungu, kama akimleta mmoja, anataka mwingine, mwingine, mwingine, mwingine, mwingine, hakuna mwisho kwake, anaendelea tu kupanda juu. Mnaona, tunataka kuwa na shauku na matarajio, Mungu anatutaka tuwe hivyo.

60 Halafu nawatakeni mwone jambo lingine, tai huufanya upya ujana wake. Je, mlijua hilo? Tai kweli huufanya upya ujana wake. Sasa, atazeeka sana hata hawezi kuruka, na ndipo mara moja jambo fulani linampata, sasa, yeye ni wa umri ule ule, bali anajisikia kuzungukwa na hisia za u—ujana, naye anajirejesha tu, yeye ni tai mzuri tena. Sasa, Biblia ilisema ya kwamba tai hufanya upya ujana wake.

61 Nami ninakumbuka mara ya kwanza nilipopata kuhudhuria mkutano wa Kipentekoste, ilikuwa ni huko Mishawaka, nilikuwa mhubiri kijana Mbaptisti, nami, huko juu, ndipo nikawasikia watu hawa, walikuwa na mabango nyuma ya magari yao, nami nikawaza, "Ninaamini nitaenda tu, ni mkutano wa kidini." Basi nikaketi nyuma ya mkutano, nami nikawasikia huko juu wakihubiri, loo, jamani, sijawahi kusikia mahubiri kama hayo maishani mwangu mwote.

Basi usiku huo, nikawaza, "Ninaamini nitaingia jukwaani."

Wakasema, "Wahubiri wote waje jukwaani." Kulikuwa na mamia yao.

62 Na kwa hiyo mimi, siku hiyo nilikuwa nikiwaona wahubiri wote vijana wakihubiri kuhusu yale Yesu aliyokuwa amefanya, na yote kuyahusu, na—na, loo, nilifikiri walikuwa na ujumbe mzuri sana, sikuwa nimewahi kuusikia huo hapo kabla. Nao wangenena kwa lugha, na kupaza sauti, na kucheza, na kukimbia kote kote, nikawaza, "Whiu! Wana tabia mbaya, lakini wao—lakini hakika wana wakati mzuri nayo, kwa hiyo na—nadhani hilo ni sawa."

63 Kwa hiyo, usiku huo, jukwaani, akasema, "Ninataka kila mhudumu asimame tu, aseme anakotoka, jina lake ni nani."

64 Kwa hiyo ilipofikia wakati wangu, nikasema, "William Branham, mwinjilisti, Jeffersonville, Indiana, Mbaptisti," nikaketi chini.

65 Ndipo basi wakamleta usiku huo, kwa ajili ya mkutano wa usiku, mzee mweusi huko nje, maskini koti kubwa mno, refu, la mhubiri lenye mkia kama tulilokuwa tukitumia huko kusini, ukosi wa mahameli, mzingo mdogo tu wa nywele nyeupe kukizunguka kichwa chake, maskini mzee huyo angeweza kwenda huko kwa shida. Anasema, "Veema, miye nitawaambia." Anasema, "Nitachukua somo langu usiku wa leo," ninaamini lilikuwa kutoka Ayubu 7:27, ama kitu kama hicho, "Ulikuwa wapi, nilipoweka msingi wa ulimwengu? Nionyeshe mahali ulipofungiwa. Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipopaza sauti kwa furaha?"

66 Ndipo nikawazia, "Jamani, kwa nini wasiwaweke baadhi ya hao jamaa wadogo huko nje? Mzee, kama huyo, mbele ya watu kama elfu tatu? Vema, hawapaswi kumweka mzee huyo huko nje, amekakamaa sana hata angetembea kwa shida."

67 Sasa, ndugu wote walikuwa wakisimulia kile kilichokuwa kimetukia hapa duniani, alianza huko nyuma yapata miaka elfu kumi kabla ulimwengu haujaumbwa, wakati wana wa Mungu walipokuwa wakipaza sauti kwa furaha, na nyota za asubuhi zilipokuwa zikiimba pamoja, akampitisha Yeye angani, na kumshushia kwenye upinde mlalo wa mvua katika yapata dakika tano. Moja kwa moja akaruka juu hewani, na kusema, "Whoopee!" Akagonganisha tu miguu yake, kisha akainama pale, na kusema, "Mna nafasi ya kutosha hapa juu kwangu kuhubiri," akaondoka jukwaani.

68 Nikasema, "Ndugu, hicho ndicho ninachotaka. Kama kitamfanya mzee atende namna hiyo, kingenifanyia nini mimi?" Nami nilikuwa na yapata umri wa kama miaka ishirini na mitano.

69 Nawaambia, kinaufanya upya ujana wake. Hiyo ni kweli? Roho Mtakatifu anapoingia, huwafanya wazee kutenda kama vijana, naam, wamekuwa tai, kuna jambo fulani kuwahusu. Sisahau hilo kamwe.

70 Hata afadhali nikanukuu hapa. Usiku huo nililala huko nje kwenye shamba la mahindi, nami nikachukua maskini ninii yangu. . .Nilikuwa na Ford kuukuu ya Muundo-T, ingeenda maili thelathini kwa saa: kumi na tano *huku* na kumi na tano *huku*. Kwa hiyo, nami nikaondoa kiti cha nyuma, na kiti cha mbele, na kuweka maskini suruali yangu yenye milia katikati yake, na kuinyosha. Nilikuwa tu na dola moja na senti hamsini za kurudi nyumbani, nikajinunulie petroli, nikanunua skonzi zilizochacha, na—na nikanunua maji, kitu cha kula.

71 Nami nikaomba usiku kucha, nikasema, "Bwana, sijawahi kuona watu kama hao maishani mwangu, sijasikia kuhusu wa namna hiyo. Sasa, siendani na adabu zao, kwa sababu hawana adabu yoyote." Lakini nikasema, "Mimi, lakini hakika nafikiri wao ndio watu wenye furaha sana, hawaionei haya dini yao."

72 Na kwa hiyo kesho yake asubuhi, nikaingia, nikaketi chini, nimevaa maskini T-shati, mwajua, na suruali yenye milia; sisi Wabaptisti, hata tulivaa ukosi uliopinduliwa, mwajua, kwa hiyo sisi—kwa hiyo tukafika kule juu, mwajua, kwenye nyakati hizo, kwa hiyo mimi. . .Nikaketi chini pale, na nikaketi karibu na ndugu mweusi.

73 Sasa, iliwabidi kufanya mkutano wao, hiyo imekuwa miaka kadhaa iliyopita, basi wakaufanyia kaskazini kwenye mkutano wao mkubwa, madhehebu mawili ama matatu mbalimbali ya Wapentekoste yalikuwa yakifanya mkutano wao mkubwa. Nadhani wameungana sasa, waliitwa P. A. ya W, na P. A. ya J.

C., ama, nafikiri linaitwa United Pentecostal Church sasa. Kwa hiyo basi. . .Nafikiri hiyo ni kweli.

74 Kwa hiyo hata hivyo, wao. . .Nilikuwa nimeketi, ninii, kule nyuma, nami nikaketi karibu na ndugu mweusi. Na kwa hiyo jamaa huyu kijana akaja, jukwaani, akasema, “Nanii, mhudumu yule kijana aliyekuwa jukwaani jana usiku, jina lake ni Branham. Alikuwa mwinjilisti, Mbaptisti, tunamtaka alete ujumbe asubuhi ya leo.”

75 Loo, jamani! Nikainama kitini, sijawahi kuwa mbele ya maikrofoni maishani mwangu, wala si—sikujua la kufanya, na suruali yenye milia na T-shati, nikainama tu chini.

76 Kwa hiyo katika dakika chache, akalitangaza tena, na kusema, “Mtu yeyote aliye nje, mhudumu kijana jina lake William Branham,” kasema, “mwambie aingie, tunamtaka alete ujumbe asubuhi ya leo.” Wakaimba wimbo mwingine na kungojea, nikachuchumaa tu chini kabisa.

Ndipo ndugu huyu mweusi akaniambia, “Je, unamjua?”

“*Loo!*” Nikasema, “Naam, bwana.”

Kasema, “Nenda ukamlete.”

Kisha nikasema, “Angalia, ndugu, njoo hapa, shikilia.” Nikasema, “Mimi ndiye.”

“Loo, ni wewe?”

Nami nikasema, “Naam, mimi ndiye.”

Akasema, “Vema, nenda huko juu.”

Nikasema, “T-shati na suruali ya milia?”

Akasema, “Hao watu hawajali jinsi unavyovalia.” Kasema, “Kwea kule juu.”

Nikasema, “La, la.” Nikasema, “*Shh*, tulia, usiseme kitu juu yake.” Mnaona, namna hiyo.

Akasema, “Kuna mtu aliyemwona William Branham?”

Kasema, “Huyu hapa! Huyu hapa! Huyu hapa!”

77 Nikajisikia kiajabu nimevaa suruali ndogo ya milia, T-shati, nilikuwa na nywele za kutosha kuchanuliwa kidogo wakati huo, mwajua. Kwa hiyo, nikaenda jukwaani, nami nikawazia, “Nitasema nini? Watu hawa wote wana furaha sana namna hiyo.” Wala kamwe sisahau nilichukua somo langu kutoka katika Ayubu. Wala mimi si. . .Samahani, nilichukua somo langu kutoka katika Luka: *Yule Tajiri Aliinua Macho Yake Kuzimuni, Kisha Akalia*. Nami nikasema, “Hakukuwako na watoto kule, ndipo akalia.”

Mtu fulani akasema, “Amina!” Sikuwahi kusikia hilo hapo awali nilipokuwa nikihubiri.

Kisha kasema, nikasema, “Hakukuwako na maua kule, ndipo akalia. Hakukuwako na Mungu kule, ndipo akalia.”

Wakaanza kusema, "Amina! Amina!"

Nami nikaendelea tu kusema, "Hakuna maua, wala hakuna watoto kule, hakuna Wakristo kule, kisha akalia, ndipo akalia, na halafu . . ." Ndipo nikalia.

78 Loo, Mungu ni wa ajabu, sivyo? Hufanya upya ujana wetu, Yeye hufanya upya ujana wetu kama tai. Sasa, tai ni ndege mkubwa. Ningeweza kukaa juu ya hili mpaka asubuhi, kuhusu tu tai.

79 Moja ya mambo ya kuhuzunisha sana niliyowahi kuona, niliwazia, maishani mwangu: nilikuwa Cincinnati si muda mrefu uliopita, yapata miaka mitatu ama minne iliyopita, nami niliwapeleka watoto wangu kule wapate kuona bustani ya wanyama. Basi ni—nilikuwa na jamaa zangu wadogo, nami nilikuwa nikiwaongoza kila mahali, nikiwaonyesha bustani ya wanyama wakati mama akileta chakula cha kutwa mezani, nasi tulikuwa na matembezi ya Jumamosi alasiri. Ndipo nikashuka kwenye kizimba kikubwa, na hapo nikaona kitu fulani!

80 Sikuzote nilimhurumia mnyama yeyote aliyefungiwa. Hata siwezi kuwa na kurumbizi nyumbani mwangu. Mnaona? Sipendi kuona chochote kilichofungiwa. La, bwana. Sipendi chochote katika utumwa, ninaamini katika uhuru.

81 Nami huenda kwenye bustani ya wanyama na kuwaona hao simba wakitembea sakafuni. Basi nilipokuwa Afrika walinipa maskini simba wawili wadogo wa kufuga, nami ningaliweza kuwaleta huku, lakini nikasema, "Kama . . ." Kasema, "Nitafanya nini nao?" Kasema, "Mwingine . . . Katika mwaka mmoja watakuwa jamaa wakubwa mno."

Kasema, "Waweke kwenye bustani ya wanyama."

Nikasema, "Waachilieni, mumu humu jangwani." Kamwe sitaweka chochote gerezani, sipendi kitu chochote kifungoni.

82 Na kwa hiyo, nilikuwa nikitembea huku na huku, nao walikuwa ndio kwanza wamemkamata tai mkubwa, ndege mkubwa mno, mzuri, naye alikuwa amemweka kwenye kizimba hiki. Na jamaa huyo, manyoya yote yaling'olewa usoni na kichwani mwake, mabawa yake yote yalikuwa yameng'olewa namna *hii*. Nami nikasimama na kumtazama, naye angerudi humo kizimbani, angerudi namna *hii* tena, angeanza, na kuyapigapiga hayo mabawa makubwa, naye angejigongesha kwenye kizimba hicho, na kuanguka tena namna *hiyo*, alale humo na kuangalia juu angani, macho hayo yaliyochoka yaangalie kote.

83 Kwa nini? Loo, yeye ni ndege aliyezaliwa mbinguni, anaishi mbinguni. Asingeweza kujiweka huru, alikuwa hana matumaini kabisa. Mtu fulani amemshika, jamaa fulani mwerevu alimshika na kumweka mle ndani. Ameyapigapiga manyoya ya mbawa zake yakatoka, ameyapigapiga manyoya ya kichwa chake

yakatoka, amelala mle kichalichali, hayo macho makubwa yakiangalia kule juu mahali pake hasa. Jinsi alivyotamani kuwa huru, na kutandaza mbawa zake kubwa, na kuruka angani, akipiga mayowe! Kwamba alikuwa…Apate kuwa huru tena! Angeweza kuangalia, bali alikuwa katika kizimba.

84 Nikawaza, "Hilo ndilo jambo la kusikitisha sana nililopata kuona maishani mwangu!" Nikawazia, "Kama wangeniuzia, ningemnunua huyo tai sasa hivi na kumwachilia, kama ilinibidi kufa nusu kwa njaa na kupunguza posho ya watoto wangu mezani kumlipia huyo tai nipate kumwachilia." Wasingeniuzia.

85 Nami nikashuka nikaenda kule na kuketi pale, nisingeweza kujizuia kulia, ndipo Kitu fulani kikaniambia, "Umeona mabaya kuliko hayo, kuwaona watu waliozaliwa kuwa wana wa Mungu, wamefungwa pingu kwa kanuni za imani, na madhehebu, na—na watu wanaosema siku za miujiza zimepita, wakati kwa kweli alizaliwa apate kuwa tai wa kuruka katika Nuru za Mbinguni kule, ndugu, chini ya nguvu na nguvu zisizo za kawaida za Mungu, kutembea kwa imani wala si kwa kuona, na jamaa fulani mwerevu amemkamata na kumfungia katika kitu fulani kwa kanuni ya imani ama kitu fulani, 'Rudia kanuni hii ya imani na hilo tu ndilo unalopaswa kufanya.'"

86 Loo, ndugu, kumtoa mtu huyo kizimbani! Kuwaona wana na binti za Mungu wamefungiwa kizimbani, ni—ni huzuni, jambo la kuhuzunisha sana nililopata kuona ni kujua ya kwamba wanaume na wanawake waliozaliwa…kuona wanawake wakitembea barabarani nusu uchi wamevaa maskini nguo hizi za kale hapa, na kujua ya kwamba mwanamke huyo amepagawa kabisa na pepo mchafu. Hiyo ni kweli.

87 Dada, hebu nikwambie jambo fulani, unasema, "Mimi ni safi kama yungiyungi, ninazivaa."

88 Lakini unatambua jambo fulani, hebu nikwambie, kwenye Siku ya Hukumu utawajibika kwa kufanya uzinzi, Biblia ilisema, "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye tayari moyoni mwake."

89 Huenda ukawa safi kama yungiyungi, bali ukijivalia hivyo, na watu wenye dhambi wa ulimwengu wakuangalie, itambidi kuwajibika kwa kufanya uzinzi *na wewe*, nawe utawajibika kwa kujianika vivyo hivyo mbele zake. Hiyo ni kweli. Maskini nguo hizi chafu, za kizinifu ambazo wanawake huvaa! Na inaingia kwenye safu yetu ya Kipentekoste, pia. Ni vibaya sana. La, bwana, kamwe usifanye hivyo.

90 Mama mmoja aliniambia, nilisema kitu kama hicho wakati mmoja, mwanamke huyu akaniambia, kasema, "Vema, Ndugu Branham, hawauzi nguo za aina nyingine yoyote ila za aina hii."

Nikasema, "Wangali wanauza vitambaa na wana cherehani, hakuna udhuru hata kidogo."

91 Hiyo ni kweli, ndugu, wakati moyo huu wa kale unapokuwa katika upatanifu na Mungu *pale*, na hiyo roho ya tai inaanza kupaa juu, unapanda juu ya mambo hayo ya ulimwengu. Shida yake ni kwamba hatuhudhurii mkutano wa maombi, na kuhudhuria kanisa, na kufanya yaliyo mema, tunakaa nyumbani kuona mchezo wa sinema, ama kitu kama hicho kwenye televisheni zetu, vipindi hivyo visivyokaguliwa, baadhi ya hiyo mizaha michafu, na kadhalika, wanayofanya, na hilo ni jambo baya kuweka mbele ya kizazi chetu cha vijana. Ninii . . . Ilikuwa ni makosa kwa watu, watu wa utakatifu, kwenda kuona sinema, ibilisi akawafanyia ujanja, akaziweka moja kwa moja nyumbani. Hiyo ni kweli kabisa.

92 Loo, ni vibaya sana. Lakini, ndugu, hebu niwaambie, ni . . . huenda wakakuweka kwenye kizimba, bali ungali ni tai. Ninaweza kuwaambia kuna njia ya kuepukia usiku wa leo. Naam, kweli. Naam, bwana.

93 Hilo, mwajua, inatupasa ku—kumchunguza tai kidogo tu. Tungeweza kukaa juu yake kwa saa nyingi, lakini hebu tumchunguze tai huyu kwa muda kidogo tu tuone alivyo.

94 Sasa, inasikitisha kuona jambo hilo. Wana na binti wanazaliwa kuwa wana na binti za Mungu.

95 Hapa juu Iowa, si muda mrefu uliopita, kusimama kwa sekunde moja tu tena, mimi, jamaa fulani alinipeleka kwenye chakula cha kutwa, naye akatoka nje na kuangalia, akasema, alikuwa nanii, alifuga nguruwe, hilo ni halali, hilo ni sawa kama akitaka kufanya hivyo. Akasema, "Nina kundi bora kuliko yote ya nguruwe katika nchi hii." Akasema, "Kundi hili, baba yangu alilianzisha, alitulea sisi sote watoto, akaniachia hilo kundi. Nimewalea watoto wangu wote, nitawaachia hili kundi," na kadhalika.

Nami nikasema, "Hilo ni sawa kabisa, bwana." Mimi . . .

Akasema, "Ni—ninamiliki mali hii yote . . . " [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

96 . . . hakuna nyoka angeweza kuupanda, huku juu kabisa mahali hapa, ndipo atatoka aende akatafute majani mabichi ya miiba, kisha arudi na kujenga kiota vilivyo, kuhakikisha kwamba hakuna upepo utakaokivumia, kwa sababu kimetiwa nanga kwenye mwamba.

97 Loo, jamani! Napenda hilo. Mungu hulijenga Kanisa Lake huku limetiwa nanga mwambani. "Juu ya mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu." Limetiwa nanga kwenye mwamba huu. Yeye ndiye Jiwe kuu la Pembeni.

98 Na wakati anapojenga kiota chake huko juu, basi, sasa, chote kimejaa miiba, kwa hiyo sasa, mama tai, atakuwa na hakika ya kwamba watoto wake watakuwa na ma—mahali pazuri pa kukaa, kwa hiyo anatoka na kuokota kila kitu awezacho.

Atamwua sungura, ale nyama, achukue hayo manyoya na kuyachomeka katika sehemu hizi ndogo, kila mwanya mdogo, na kukikaza, mpaka kimekazwa vilivyo, nadhifu kiwezavyo kuwa wakati—wakati kiota kimekamilika.

99 Sasa, yeye, anajiandalia nini? Anajiandaa kwa ajili ya watoto wake. Naye anawataka wawe na mahali pazuri, padogo, laini pa kutembea, na kadhalika, yeye anawashughulikia. Jinsi Mungu anavyowatendea watoto Wake vivyo hivyo! Loo, jinsi anavyobariki moyo wetu! Wakati hao tai wadogo wanapozaliwa, kiota kidogo laini cha kutembelea.

100 Unakumbuka mara ya kwanza ulipozaliwa mara ya pili? Roho Mtakatifu alipokuja kwako, nawe ukawa Mkristo, ulijisikia kama ulikuwa tu unatembea juu ya manyoya. Sivyo?

101 Ninakumbuka nilipookoka mimi, mbona nilikuwa yapata yadi arobaini kutoka nyumbani, ubao wa kutembelea umefika kule juu, nami nawaambia, siamini niliwahi kugusa huo ubao nikiingia.

Ndipo Mama akasema, "Una shida gani, Billy?"

Nikasema, "Sijui kabisa, Ma. Kamwe siwezi kukwambia."

102 Nami ni—nikachukua Biblia yangu, nisingeweza kuisoma, nikachukua kitabu cha nyimbo, nisingeweza kukisoma, nikakiweka chini na kuzunguka nyuma ya nyumba, kulikuwa na njia ya reli huko nyuma, nami nikaingia kwenye njia hiyo ya reli, na ilinibidi kutoa mvuke mahali fulani, nilikimbia kwenye hiyo reli kwa nguvu nilivyoweza, na nikaruka juu kabisa hewani na kupaza sauti, "Whoopee!" kwa nguvu tu nilivyoweza. Ilinibidi kutoa hisia hiyo. Loo, nilikuwa nikielea hewani. Jamani, huko kuzaliwa upya!

103 Wakati maskini tai huyu anapokuja, loo, yeye ni, anapenda makazi yake. Sasa, mama tai anaenda na kuleta samaki, na analeta sungura, na analeta kondoo ama chochote anachoweza kupata, na anamwandalia maskini tai huyu mlo mzuri; awe na hakika ya kwamba kadogoo atapata kitu kizuri.

104 Nina furaha sana kwamba Yehova huhakikisha ya kwamba maskini tai wake wadogo wanapata Chakula kinachofaa. Yeye atakiweka mbele yako, kama unataka kukila au hutaki, itakubidi kugeuza kichwa chako, lakini kama wewe umezaliwa tai, "Kondoo Wangu, tai Wangu, wanaijua Sauti Yangu." Wanajua Chakula.

105 Kasema, "Unanipenda, Petro?" Kasema, "Lisha kondoo Wangu." Ninapenda hilo, "Lisha Kondoo Wangu."

106 "Lisha Kondoo Wangu," usiwafukuze, walishe. Walishe Neno, wanapenda Chakula cha kondoo. Mwajua, watu wengine hawakipendi Chakula hiki cha kondoo. Chakula cha kondoo ni ile hisi nzuri ya kale ya wokovu wa kale, huru tu uwezavyo kujisikia, wala hakuna hukumu.

107 Mbona, tulikuwa tukisimama, na kupiga makofi, na kuimba, "Nilijisikia vizuri, hakuna hukumu moyoni mwangu," nikiwa na wakati mzuri sana.

Na bila shaka, itawafanya hao kuku wadogo kuangalia juu, waseme, "*Chwi, chwi, chwi*, *chwi*, *chwi!* Ulokole."

108 Kulikuwako na mkulima si muda mrefu uliopita, alikuwa mkulima mwenye kutaka makuu, hakuwa na ghala kubwa sana, bali alikusanya tu mazao mazuri, na kufanya kila kitu alichoweza kutunza mifugo wake. Jamaa mwingine alikuwa na matrekta mazuri, lakini alikuwa mvivu sana ku—kulima. Vema, majira ya kupukutika yalipokuja, yeye—yeye alikata magugu yake na kuyaweka ghalani, alikuwa na ghala zuri, loo, jamani, ghala zuri. Lakini jamaa huyo mwingine, hakutumia wakati kwa hilo zizi, bali alikuwa akihakikisha ya kwamba, wanyama wake wamepata chakula kizuri.

109 Kwa hiyo, kulikuwako na ndama aliyezaliwa katika kila zizi, ndipo—ndipo mwaka uliofuata wakati majira ya kuchipua yalipofika, mwajua, ni—ninii, labda yule ndama aliyezaliwa kwenye lile zizi zuri, kubwa mno, minara mirefu, mwajua, na viti vya kifahari, mnajua ninalozungumzia, kwa hiyo mnaweza kusoma katikati ya mstari, bali hakuwa na chakula kingi.

110 Kwa hiyo basi, wakawafungulia, wote wawili wakawafungulia, wakapata upepo kidogo wa majira ya kuchipua. Loo, jamani, maskini ndama huyu alikuwa katika misheni ndogo kule chini, mahali fulani, kanisa dogo, mwajua, a—alikuwa amenona kabisa, na mnene, na amejaa vitamini, jamani, akatoka huko nje, nao upepo huo ukaanza kuvuma juu yake, alikuwa amejaa nguvu, akaanza kurusha mateke yake na—na kurukaruka huku, huku, huku, mbona, alikuwa anajisikia vizuri.

111 Wakamtoa yule ndama mwingine, aliyekuwa amelishwa magugu ya kikanisa, mwajua. Alipofika huko nje, maskini jamaa huyo, upepo ulikuwa karibu umwangushe chini, akiyumbayumba kote namna *hiyo*. Ndipo akauchomeka maskini uso wake kwenye ufa wa ua, akachungulia, na kumwona ndama huyu mdogo akifurahi tu na kurukaruka, akirukaruka kila mahali, kasema, "*Tsk*, *tsk*, *tsk*, *tsk!* Ulokole kama huo!"

112 Loo, napenda kula Chakula cha kondoo, Chakula kizuri, nguvu za Mungu, Neno la Mungu, Roho Mtakatifu hula Hilo. Hilo ndilo Kanisa linahitaji usiku wa leo, ni mahubiri mazuri, imara ya Injili, Mafundisho ya Injili, wokovu wa Injili, na Roho Mtakatifu wa Injili. Amina. Hatuvutiwi sana na . . . Vema, taifa hili huenda lisihitaji Rais mpya, huenda jiji hili lisihitaji meya mpya, bali tunachohitaji siku hizi ni uamsho mzuri wa kale wa Mtakatifu Paulo na Roho Mtakatifu wa Biblia kurudi kanisani tena. Hicho ndicho tunachohitaji, kondoo wanaolishwa Chakula cha kondoo, si magugu ya kikanisa.

113 Sasa, kiota hiki kidogo kiliundwa kabisa, ndipo akamletea cha—chakula, naye akala, na loo, jamani, alikuwa akikua. Sasa yeye, muda si muda mwajua, ameanza kumea manyoya, mwajua, anaanza kuingia katika kazi ya pili ya neema, naye a—anaanza kumea manyoya vizuri sana, mwajua.

114 Kwa hiyo mama tai anaanza kuangalia chini, naye anaanza kuwazia, "Unajua, sitaki kamwe watoto wangu wawe kuku. Hivyo tu." Mnajua, Mungu amekusudia tu jambo hilo, na Yeye hataki tuwe kuku wa ardhini. Kwa hiyo mama tai akasema, "Sina budi kulishughulikia jambo hili." Kwa hiyo, muda si muda mwajua, hana budi kuwatoa hao tai kwenye kiota hicho, hivyo tu, wakikaa mle watakuwa wa duniani.

115 Na hivyo ndivyo ilivyo. Wewe ninii tu...Mara nyingi nimeshangaa ni kwa nini tuliondoka na kupata elimu kubwa ya kusomea, kuwa mhubiri, halafu tunakuja na historia yote ya kanisa, na *haya* yote, na vitamini zote, na kila kitu, kisha tunageuka na kusema, "Vema, bila shaka, siku za miujiza zimepita."

116 Unawezaje kumwona mtu anayeganda hata kufa, unawezaje kumyeyusha kwa moto wa kuchorwa? Vipi kama mtu anaganda, useme, "Unaona ule moto mkubwa mno uliochorwa pale? Kwenye Siku ya Pentekoste kulitokea uvumi kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi."

"Naam, ninatetemeka."

117 "Loo, Roho Mtakatifu aliwashukia, Ndimi za Moto." Loo, hilo lilikuwa ni jambo kuu, bali hilo lilikuwa huko nyuma. Mnaona, huo ni Moto wa kuchorwa, huwezi kujipasha joto kwa huo. Kama tunahitaji Moto leo hii, basi hatuwezi kupata joto kwa Moto wa kihistoria. Mungu wa kihistoria ana faida gani, kama Mungu wa Ibrahimu si Mungu yeye yule leo, Mungu wa Paulo si Mungu yeye yule leo? Kama Roho Mtakatifu aliyeshuka kwenye Pentekoste si yeye yule leo, basi tuko wapi? Sawa.

118 Ni kama kuwapa kurumbizi wako mbegu nyingi zenye vitamini ndani, na kufanya mabawa mazuri, na kumweka kizimbani wakati wote. Unaona? Hawezi kutumia mabawa yake. Kuna haja gani ya kujifunza yote kumhusu Mungu, kama ukijaribu kusema Yeye alikufa miaka elfu mbili iliyopita, na hakuna cha zaidi kwake? Ninaamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye yu hai. Naye alisema, "Kwa kuwa Mimi ni hai, nanyi mnaishi pia." Amina. Nina furaha kwa ajili ya Chakula cha tai. Hiyo ni kweli.

119 Sasa, maskini mama tai amedhamiria kwamba hawatakizoea kiota hicho kupita kiasi; na Mungu amekusudia tu kwamba mtoto mchanga aliyezaliwa upya hatazoea ulimwengu huu kupita kiasi. Hiyo ni kweli. Yeye hataki tuzoee hapa, Yeye anaenda kujiandaa kutupeleka hewani.

120 Siku chache kabla ya maskini mama tai kuwapeleka watoto wake hewani, mnajua afanyacho? Kwanza, anapanda kule juu, anasimama kwenye kiota. Na baadhi ya tai wana futi kumi na nne kutoka ncha hadi ncha, ndege mkubwa kuliko wote tulio nao. Atasimama kwenye kiota hiki, maskini tai mama kwa kawaida ndiye mkubwa kati ya wote wawili, naye atatembea huku na huko juu ya kiota hiki, naye atapiga mayowe, "*Koo!*" huo mlio ambao tai hutoa.

121 Anajaribu kufanya nini? Anajaribu kuwafundisha watoto wake mlio wa sauti yake. Hmm! Wanaingia hatarini katika muda mfupi, kwa hiyo hawana budi kujua mlio wa sauti ya mama. Loo, nawaambia ni muhimu kuisikiliza Sauti ya Mungu, ile Sauti ndogo tulivu inayonena kwa kina na kwa utajiri, inavutia usikivu wa watu Wake.

122 Naye anatembea huku na huku juu ya kiota hiki, na halafu, wakati mwingine, atakunjua mbawa hizo kubwa mno, azipigepige huku na huku. Ndipo hao tai wadogo wataninii, kwa namna fulani itawatikisa tu kidogo, mwajua, nao wataangalia nyuma, na "Loo, Mama, jinsi ulivyo ndege mashuhuri!"

123 Loo, ninapenda tu hilo, kwa sababu Mungu ana mabawa mawili, Agano la Kale na Agano Jipya. Anayakunjua, nasi tunayaangalia, na kuangalia juu, na kusema, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu!" tunaposikia ya kwamba Yeye aliifungua Bahari ya Shamu na kuwavusha wana wa Israeli, Yeye alimfufua Lazaro katika wafu, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, Agano Jipya na la Kale, Mungu yeye yule, Yehova yeye yule, Roho Mtakatifu yeye yule moja kwa moja Kanisani leo hii, akienda huku na huko.

124 "Mnaona jinsi nilivyo mkuu? Mimi ni yule yule aliyemkomboa Musa, mimi ni yule yule aliyemkomboa Danieli, mimi Ndiye, aliyewatoa wana wa Kiebrania kutoka kwenye ile tanuru iliyowaka moto, mimi Ndiye niliyekuwa huko Sodoma na Gomora, mimi Ndiye niliyezungumza na Ibrahimu. Loo, MIMI NIKO AMBAYE NIKO. MIMI NIKO." Wakati uliopo! Sasa!

125 Loo, Mungu atawachukua maskini tai Wake kwa mruko wa binafsi moja ya siku hizi. Naam, bwana. Yeye anajitayarishia nini?

126 Mnaona, kamwe hawakujua kitu ila kiota, hawakujua chochote ila dhehebu au kanuni ya imani. Nao ni tai, kwa hiyo Mungu anatembea huku na huku, hata katika mkutano huu, usiku baada ya usiku, akionyesha kile alicho, Yeye ni "MIMI NIKO AMBAYE NIKO," Yeye alisema. Yeye ni Mungu, Yeye ni Yehova-Tai, akijaribu kuwaonyesha watu ya kwamba Yeye ni Ndege yule yule mkuu, mwenye nguvu.

127 Anasema, "Unaona mbawa zangu hizi kubwa mno?" Mama tai, "Sasa, ndugu yenu mkubwa zaidi, na hao wanaoruka humu

ndani kuwaona mara moja moja, niliwatoa kwenye kiota kwa mbawa hizi, niaminini mimi."

128 Loo, haleluya! Ninaangalia nyuma kwenye Pentekoste, Yeye anasukuma mbawa Zake juu kuwapa Pentekoste mnamo A.D. 33, Yeye bado anawapa watoto wangu Pentekoste leo. Amina. "Mimi ni Yehova-Tai, ninawachukua kwa mbawa za tai. Mimi ni yeye yule jana, leo . . . Mimi Ndimi niliyewatoa wale wana wa Kiebrania kutoka kwenye ile tanuru ya moto, Mimi Ndimi niliyenena na Musa katika kijiti kilichowaka moto, mimi ni yeye yule, ninawatakeni mtoke. Kama wewe ni mgonjwa, kama wewe ni mhitaji, ninakutaka utoke. MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Mimi ni Yehova, isikieni Sauti Yangu."

129 Nisikilizeni, msichukue sauti ya kuku anayejaribu kuzungumza nanyi, ama mla mizoga fulani, Afadhali mumsikilize Mama Tai, hii ni Sauti yake moja kwa moja katika Neno.

130 Yeye atafanya nini? Sasa, mabawa haya makubwa, hawana budi kuyaamini hayo mabawa. Sasa, anawaangalia watoto wake, tangu wamekuwa kwenye kiota hiki cha kale, cha kikanisa, nao hawaonekani wazuri sana. Sasa, wana manyoya mengi yaliyolegea ndani yao, naye anajua kama akiwahi kumpeleka mmoja wa hao tai hewani, na kumwangusha kwa hayo manyoya yaliyolegea, atavunja shingo yake.

131 Na bado kuna mashaka mengi sana kanisani kuruka. Hiyo ni kweli. Ana manyoya mengi kupita kiasi ya mkiani, manyoya mengi mno yaliyolegea. Kwa hiyo mnajua anachofanya? Anawapa kazi ya tatu ya neema. Anasimama kule nyuma, na kuchukua mabawa haya makubwa, naye anaanza kuyapigapiga namna *hiyo*, ndipo upepo wenye nguvu unaoenda kasi unashuka kupitia pale, nayo manyoya yote yaliyolegea yanaanza kupukutika.

132 Loo, wakati huo upepo wenye nguvu unaoenda kasi utakapokuja kutoka Mbinguni, ubatizo wa Roho Mtakatifu, manyoya yote yenye mashaka yatakutoka. Amina. Sasa, ninajisikia wa kidini, amina, nimeanza kujisikia kuzungumza nanyi sasa.

133 Loo, wakati hizo siku za kale zenye mashaka, maskini manyoya ya kale yakitokeza mle ndani, yakisema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu."

134 Hebu upepo huo wenye nguvu unaoenda kasi kutoka kwenye hizo mbawa za Agano Jipya na la Kale uanze kuruka huku na huku, ukisema, "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele!" Jinsi maskini manyoya yote yaliyochongoka yanavyoanza kuruka! Afadhali usianze nayo ndani yako, kama utafanya hivyo, utapasukia hewani mahali fulani, kamwe hutachukua mruko huo wa binafsi.

135 Anajitayarisha. Vema, yeye huyapepea manyoya yote, aone kama yote ni mazuri na yameshika. Sasa, anajiandaa kuwapeleka hewani. Hawataki kwenda, wameridhika sana wakitembea katika kiota hicho. Kwa hiyo mnajua anayofanya baadaye? Anaruka moja kwa moja kwenye kiota hicho, na kuchukua huo mdomo mkubwa, na kuokota manyoya hayo yote, anaokota ngozi ya kondoo, anaitupa nje, na kuirusha kwenye kuta, hakuna kitu kilichosalia mle ndani ila miiba, na maskini jamaa hawa wana wakati mgumu.

136 Unajua yapata mara ya kwanza ulipopata Roho Mtakatifu, unajua, na kila mtu akaanza kukusengenya, na kukudhihaki, na kadhalika. Unakumbuka jinsi hiyo ilivyokuwa? Kila wakati alipoketi chini, ni mwiba, "*Oomph*! Uh!" na huko nyuma, wajua. Lakini Yeye hataki kuuzoea ulimwengu huu, Yeye yuko tayari kukupeleka Mahali fulani. Wakati mwingine Yeye huacha ugonjwa ukupige, anaachilia kansa, anaachilia uvimbe, ama kitu fulani kikupige aone kama uko tayari kwa kuruka hewani. Loo! Aone kama uko tayari. Yako wapi manyoya yote? Angalia kama kila kitu ni sawa. Naam.

137 Daktari aliniangalia, na kusema, "Una dakika tatu zaidi za kuishi."

"Naam, lakini kama ningesikiliza hayo, ningekuwa nimekufa miaka mingi iliyopita." Lakini Yeye alipulizia tu manyoya yote yaliyolegea *kwa namna fulani*.

138 Na maskini tai mdogo, ataanza na yeye, kila kitu ni cha mashaka, ataketi chini, "*Oomph*!" anachomwa miguu yake, naye anakuta miiba kote kwenye kiota, maskini waridi mwitu, anaiweka mle ndani kwa kusudi fulani. Nayo Biblia inatwambia ya kwamba majaribu yetu yana thamani zaidi kwetu kuliko dhahabu ya thamani, na halafu tunayazozania.

> Loo, lazima nibebwe nyumbani Mbinguni
> Kwenye kitanda chenye maua ya starehe,
> Wakati wengine walipiga vita wapate kushinda tuzo,
> Na kusafiri kupitia bahari zilizolowa damu?

139 Mbona, sisi Wamarekani, tunataka tu kuketi kitako na kuburudishwa, na kama mtu fulani akisema jambo fulani, "Aisee, nilisikia ulijiunga na watakatifu wanaojibingirisha!"

"Vema, nadhani sitarudi huko tena, mke wangu."

140 Loo, jamani, wewe ni maskini tai, huenda ukawa mwewe, bali wewe si tai, hilo ni jambo moja la hakika. Hebu nikwambie, ndugu, naam, bwana, kama wewe ni koho unakula vitu vya ulimwengu, bali tai hula nyama safi. Haleluya!

141 Tai wa Mungu hula Neno la Mungu na Hilo pekee. Hana . . . Hawezi kuvumilia kitu hicho cha kale cha ulimwengu, hiyo ni kweli, hakita—hakitameng'enyuka, asingeweza kukivumilia,

kwa vyovyote vile. Anataka nyama safi, anataka upya wa Roho Mtakatifu, nyama ya Mungu moja kwa moja kutoka kwenye Biblia. Anaitamani, atapitia kwenye dhoruba za theluji, na kila mahali. Anaposikia kuna uamsho unaoendelea, atauendea upesi awezavyo. Yesu alisema, "Palipo na mzoga, tai watakusanyika." Amina.

142 Kama wao ni Presbiteri, Methodisti, Baptisti, ama chochote walichokuwa, wakati nguvu za Mungu zinapoanza kushuka kulingana na Neno la Mungu, tai halisi wa kweli watakuja kwenye karamu hiyo, hakuna kitu ulimwenguni kinachowaweka mbali na hapo. Wataenda kwa vyovyote vile, ambapo nguvu za Mungu zinaanguka-. . . Unaweza kusema wao ni watakatifu wanaojibingirisha ama chochote unachotaka, wataenda vivyo hivyo tu, hauleti . . . maana tai wao, wao—wao hula hicho, hicho ndicho wanachokula.

143 Basi mama huyu, inafikia wakati, hana budi kukitaharikisha kiota hiki, naye anakitupa chote nje, na kutupa se—se—sehemu yote laini nje, na kuweka majaribu juu yako. Sasa, maskini mwewe angefanya nini, ameketi kwenye kiota hicho? Kamwe asingetoka humo, hivyo tu. Lakini tai, hukitaharikisha kiota chake naye yuko tayari.

144 Sasa, siku moja anasema, "Sasa nafikiri ni wakati wa kuwapeleka watoto wangu wadogo hewani." Naye anakuja akipiga mayowe hewani.

"Naam, huyo hapo Mama anakuja!" Wanajua hilo.

145 Ni kama tu Kanisa lililojazwa na Roho Mtakatifu, wakati Roho Mtakatifu anapoanza kushuka, mikono itainuliwa, "Haleluya, Yeye yupo hapa!" Amina. "Loo, nina furaha sana!" Mbona, huyu hapa jirani yako ameketi hapo, hujali ni nani aliyeketi hapo, Mama Yehova anakuja kwenye kiota. Utukufu! Hmm!

146 Jalia ashuke usiku wa leo, hebu na ayatandaze mabawa Yake makubwa mahali hapa, amtoe kila mtu kwenye kiti cha magurudumu, kila mwenye dhambi hadi madhabahuni. Atakuja amepanda mbawa za tai. Amina. Loo, najisikia vizuri! Naam, bwana, Yeye ataingia, kama utamruhusu, kama utamwalika. Unasikia kilio hicho kikija, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu. Wanaweza kujua hilo."

147 Loo, nilikuwa nikizungumza na daktari fulani si muda mrefu uliopita, naye akasema, "Billy . . . "

148 Nilikuwa na mkutano huu katika ukumbi wa shule ya sekondari huko Jeffersonville, nyumbani kwangu, ndipo watu wakaanza kupiga makelele na kumsifu Bwana, huko chini, maana mambo fulani yalitukia. Ndipo daktari akaniambia . . . Nikasema, "Waonaje kuhusu hilo, Dak?"

Naye akasema, “Billy, unajua nini? Nafikiri hao watu wamesisimkwa tu.”

Nikasema, “Wewe ni daktari, nawe unajua huwezi kusisimkwa, isipokuwa kuwe na kitu fulani cha kukusisimua.”

149 Loo, utukufu kwa Mungu! Hakika, husisimua. Ni Roho Mtakatifu anayeingia na kutusisimua, tuko tayari kuruka moja ya siku hizi kwenda Utukufuni. Hakika, inasisimua, kama hilo halikusisimua, ningelibadilisha kwa kitu kinachosisimua.

150 Ninaweza kuwathibitishia kwa sayansi, ya kwamba chochote ambacho—ambacho hakisongi kimekufa. Hiyo ni kweli. Mnajua, kama mtoto mchanga amezaliwa wala halii, hatoi kilio kikali, ha—hafanyi chochote mtoto huyo amekufa. Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, tuna watoto wengi mno waliozaliwa wamekufa. Unajua yale daktari hufanya kwa kawaida? Anamnyakua kwa visigino, na kumpa kichemsho kidogo cha makalio, ambacho humlainisha vizuri kabisa.

151 Basi kile Kanisa linachohitaji leo hii ni kichangamsho kizuri, cha kale cha nguvu za Roho Mtakatifu kuja Kanisani, kuturarua, na kututikisa, kukitaharikisha kiota, na kulipulia mbali manyoya yaliyolegea. Pentekoste inahitaji kutaharikishwa. Amina. Kupulizia mbali manyoya yaliyolegea, tunapata mashaka mengi sana miongoni mwetu, ushirikina, na “Yaweza kuwa hivyo? Je, itakuwa hivyo?”

152 Hakika, ndivyo ilivyo, Neno la Mungu lilisema ndivyo ilivyo, Chakula cha tai kinathibitisha kwamba ndivyo ilivyo. Amina. Hakika, ndivyo ilivyo. Tai-Yehova anaingia, anataharikisha kiota, kanisa linapata pia, lime—limetuama. Naam. Afadhali uingie ukalitaharikishe.

153 Vema, unasema, “Ndugu Branham, tayari nimepata Roho Mtakatifu.”

Naam, lakini wanapata manyoya yaliyolegea mle ndani. Unaona?

154 Nilikuwa nimesimama kando ya bahari wakati mmoja, ilikuwa ni Ziwa Michigan, hasa, mahali ilipokuwa, nami nikaona kitu hicho, maji yakiingia kwa kishindo, na kutoka kwa kishindo. Nilisimama pale na kuwaza, “Mafuriko ya furaha juu ya nafsi yangu, kama mawimbi ya bahari yakifingirika.” Nikaanza kuwazia, nikawaza, “Unajua nini hata hivyo? Hakuna tone moja zaidi la maji katika bahari hii, ama, ziwa hili, kuliko ilivyo wakati limetulia kabisa.”

155 Hiyo ni kweli, lina kiasi kile kile cha maji, lakini linaruka na kupiga makelele. Nikawaza, “Vema, kwani kuna nini? Lina uamsho unaoendelea. Huo unafanya nini? Unaoshea takataka zote ufukoni.”

156 Huo ndio tunaohitaji leo ni uamsho mzuri wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu kuondoa shaka na takataka mioyoni

mwetu, uzifagilie ufukoni, uzisahau, amina, kuisafisha bahari. Amina. Hicho ndicho tunachohitaji, maskini mshindo mzuri wa kale.

157 Ninapenda kitu chenye uhai, kinachosonga. Nilikuwa mlinzi wa wanyama wa jimbo huko Indiana, nilikuwa nikipita karibu na chemchemi, hiyo ilikuwa ndiyo chemchemi nzuri sana niliyopata kuona, majira ya kiangazi ama baridi kali, kila mara, *bubujika*, *bubujika*, *bubujika*, *bubujika*. Nikawaza, "Vema, unajua, hicho ndicho kitu chenye furaha kuliko vyote nilichopata kuona." Niliketi chini siku moja, kisha nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani, Bw. Chemchemi. Kwa nini una furaha hivi? Unabubujikia nini wakati wote? Kwani una furaha sana kwa sababu sungura wanakunywa kutoka kwako?"

"La," angesema, kama angeweza kuzungumza.

Nikasema, "Vema, basi una furaha kwa sababu, labda, kwamba mifugo wanakunywa kutoka kwako?"

"Hapana."

Nikasema, "Ni kitu gani kinachokufanya ububujike basi? Kwa sababu ninakunywa kutoka kwako?"

Angesema, "La, Ndugu Branham, si hilo."

Nasema, "Ni kitu gani kinachokufanya ububujike?"

Angesema, "Si mimi ninayebubujika, ni kitu fulani nyuma yangu kinachonibubujisha."

158 Hivyo ndivyo ilivyo. Hicho ndicho Kanisa linachohitaji siku hizi, ni Roho Mtakatifu nyuma yao kububujisha kidogo, kutupilia mbali kutokuamini huko, na takataka, na ma—mawazo kwamba siku za miujiza zimepita, na kadhalika. Hebu na tuzirudie nguvu kuu za Yehova, Chakula kikuu cha tai cha Yehova, na kuamini ya kwamba sisi ni watoto wa Ibrahimu, tai wa Mungu walioitwa. Tuirudie Injili, tulirudie Neno, tuirudie kweli, tukirudie Chakula, Chakula cha Malaika, Chakula cha wana wa Mungu.

159 Tai anakitaharikisha kiota chake akijiandaa kwa ajili ya kuruka. Naam. Loo, ni vizuri sana kujua mambo haya! Basi muda si muda mwajua, maskini mama tai anapanda pale naye anapiga mayowe, nao wanaijua sauti yake. Kisha anashuka kwenda mahali walipo hao tai wadogo, na anawahutubia, "Mnajiandaa kuruka sasa. Jambo fulani liko karibu kutukia, ila msiogope kama mnaniamini."

160 Kama vile Ibrahimu jana usiku, "Njoo huku, umchukue mwanao mwenyewe, umpeleke hapa juu ya mlima, na kukata koo lake. Utaniamini Mimi?"

"Ninakutumaini, Bwana," akasema Ibrahimu. Loo, jamani!

161 Jambo fulani lilikupata, ukawa mgonjwa, jambo fulani likatukia, *hili* likatukia, mtu fulani alikufanyia mzaha, bosi

alisema atakufuta kazi kama angekupata ukiomba tena; Atakujaribu aone kile ulicho. “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa na kurudiwa.” Jambo ndilo hilo. “Na endapo hamwezi kustahimili kurudiwa, mnakuwa watoto haramu, wala si watoto wa Mungu.”

162 Mtu anapokuja, sijali, huenda akapaza sauti, huenda akanena kwa lugha, huenda akatabiri, huenda akafanya lolote atakalo, na kama akiingia katika jaribio hilo kisha arudi nyuma, yeye si mwana wa Mungu. La, bwana. Kama itachukua maisha yake, yeye anasimama pale vivyo hivyo, kwa sababu anajua ni nani aliyemwamini, na ameshawishika ya kwamba anaweza kukilinda kile alichoweka amana Kwake kwa ajili ya ile siku. Amina.

163 Sasa mama tai anasema, “Jiwekeni tayari, enyi watoto, nitawapa mruko wenu wa kibinafsi asubuhi ya leo.”

164 Kwa hiyo anatandaza mabawa yake makubwa, na kila mmoja wa hawa tai wadogo anapanda juu ya hayo mabawa makubwa. Loo, ninapenda hilo! Juu ya Agano Jipya na la Kale yote mawili. Wanapanda juu yao namna *hiyo*, na kusema, “Vema, kaza kabisa mshiko wangu.” Ananyosha mdomo, anashika moja ya hayo manyoya makubwa mno ambayo usingeweza kuyang’oa kwa koleo, anaweka maskini mdomo wake pale, na kuyashika mle ndani, maskini mshiko wake pale, anachukua makucha haya madogo, anayachomelea kwenye mabawa, na kusema, “Vema, Mama, niko tayari.” Loo, jamani!

165 Yehova nani? Mwenyezi Mungu, El Shaddai, Mwenye matiti, yule Tai mkubwa, Mwenye mabawa, Biblia, Agano la Kale na Jipya. Shikilia tu, chochote unachohitaji, shikilia moja kwa moja kwenye ahadi ya Mungu, na uketi papo hapo, haidhuru ni jambo gani linalotukia, shikilia. Ushikilie mkono wa Mungu usiobadilika.

166 Umefikia juu. Kisha ukasema, “Mimi ndimi Bwana, akuponyaye magonjwa yako yote.” Ishikilie. Kama Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ishikilie. “Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa.”

167 Mchungaji anasema, “Hakuna kitu kama hicho siku hizi.”

168 Shikilia yale Mungu aliyosema, weka ndoana yako hapo na ushikilie. Unajiandaa kuruka sasa, kumbuka, inaonekana ni hatari, shikilia. Loo, nina furaha sana! Kwani mwewe asingeweza kufanya hivyo hata afanyeje. Kuku hata hana kulabu mdomoni mwake, angeanguka kabla hajatoka kwenye kiota. Mara ya kwanza mtu yeyote aliposema jambo fulani kumhusu, angesema, “Loo vema, nadhani halikuwa sahihi.”

169 Loo, lakini tai ni ndege aliyeumbwa maalum. Anaichomelea maskini mshiko wake mdogo pale, na kutia hiyo miguu mle ndani, naye anajua jinsi ya kushikilia. Shikilia mbawa za

msalaba, ndugu, mwache, acha dhoruba zitikisike, endelea tu kusonga mbele, ukipanda juu.

170 Anatandaza mbawa hizo kubwa, anawanyanyua hao tai wadogo, anahisi uzito wao namna *hiyo*, anaruka kwa nguvu kutoka juu ya mwamba huu. Sasa, jamaa hawa wadogo kamwe hawakuhisi upepo huo hapo awali, hilo ni jambo geni kwao.

171 Mnakumbuka, mara ya kwanza mlipouhisi, enyi wana tai, ule Upepo wenye nguvu ukienda kasi ukishuka kutoka Mbinguni uliwakalia, na Ndimi zilizogawanyika kama moto zikakaa juu ya kila mmoja wao, mnakumbuka wakati ulipokugusa? Lilikuwa ni jambo la ajabu ninyi, Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, Lutheri, Katoliki, na Pilgrim Holiness, Wanazarayo, na kadhalika. Mlikuwa mumezaliwa, hakika, mlikuwa mumezaliwa mara ya pili, Mkristo kwa kuamini, lakini wakati huo Upepo ulipoanza kuja, loo, manyoya yaliyolegea yakaanza kuruka, ninawaambia, jambo fulani lilitukia, lilikuwa likiwatayarisha kwa ajili ya safari yenu.

172 Kwa hiyo maskini yule tai akashikilia. Maskini mama huyo akachukua mbawa zake, kisha akaruka kutoka kwenye hicho kiota, akaanza kupanda juu zaidi, akaingia mawinguni, loo, jamani, juu kabisa, akapaa juu, akapaa juu, juu kabisa, juu kabisa. Kama ikitokea kuna kuku mle, ameondoka wakati huo, angechanganuka tu na kuanguka, lakini hawa tai wadogo wameumbwa maalum, wanamjua Mungu.

173 Mungu alikuita, alikujua, na kukuchagua, na kuweka jina lako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ulimwengu haujaumbwa kamwe, hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Mpinga Kristo katika siku za mwisho, atawadanganya wote walio juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo ni kweli. Unaogopa nini? Panda ubebwe.

174 Usiogope, ndugu kwenye kiti cha magurudumu. Usiogope, dada. Usiogope, ndugu. Wewe uliye na kansa, ugonjwa wa moyo, ama chochote kile, usiogope. Mungu amekualika ushike mabawa ya msalaba katika Biblia hii hapa, ahadi ya Mungu, kisha uruke uingie mawinguni.

175 Kasema, "Sikuwahi kuwa huko juu hapo kabla, Ndugu Branham."

Mshikilie, Yeye atakupeleka huko juu.

"Ninawezaje kufanya hivyo, Ndugu Branham? Si—sininii . . . Kamwe sikusogeza mkono wangu, ni—ni—ni—ni . . . "

Haileti tofauti yoyote, usogeze, kwa vyovyote vile, Mungu alisema hivyo. Amina. *Brrrrr*!

176 Najua mnafikiri nina kichaa, lakini kama nikiachwa tu peke yangu, nina furaha zaidi namna hii, kuliko nilivyokuwa

vinginevyo, kwa hiyo ni—nimeridhika namna hii. Vinginevyo nilikuwa na wasiwasi, na mahangaiko, na kila kitu, sasa mimi, hakuna hukumu, ninajisikia tu vizuri. Mnaona? Kwa hiyo, napenda hili. Naam, bwana. "Kwa njia inayoitwa uzushi, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu." Hiyo ni kweli.

177 Sasa, maskini mama tai anaenda mbali sana mpaka karibu haonekani. Mnajua anachowafanyia hao tai wadogo, anapofika kule juu? Nimewaangalia mara nyingi. Anawatikisa kila mmoja waanguke.

"Loo, ewe mama katili!"

178 Loo, la! Ewe mama mwerevu. Anawatikisa kila mmoja aanguke hewani, maana haogopi. Kama walikuwa, walikuwa na ujasiri wa kutosha kuweka matumaini yao, yeye. . . Walikuwa tayari wameangalia juu ya mbawa zake kubwa, walijua alikuwa ni nani, walikuwa wamemwona, naye alikuwa amewaambia jinsi ndugu zao walivyokuwa, mwaka uliotangulia. Naye alijua walikuwa wakiruka, walijua walikuwa wakiruka. Alijua walikuwa ni tai, wala hakuogopa kuwatikisa waanguke.

179 Mungu haogopi kukuweka kwenye majaribu. Wakati alipomwambia Ayubu. . . Shetani alisema, "Loo, naam, umemzingira kabisa." Kasema, "Mfanyie. . . Vunja ua unaomzunguka, nitamfanya akukufuru mbele za uso Wako."

Akasema, "Yuko mikononi mwako."

180 Loo, jamani! Mungu haogopi kuwaweka tai Wake kwenye—kwenye jaribio la kuruka hewani. Yeye haogopi, anakutegemea wewe. Hakuogopa kumweka Ibrahimu kwenye jaribio la kuruka hewani, Alikuwa anamtegemea. Wala Yeye haogopi kuuweka Uzao wa Ibrahimu kwenye jaribio la kuruka hewani, maana Yeye anakutegemea.

181 Anawatikisa hao tai wadogo moja kwa moja hewani, akasema, "Vema, enyi watoto, papatikeni wenyewe." Hmm, jamani! Mmoja wao, mwajua, yeye. . . Basi mama anafanya nini? Anashuka kasi upande mmoja, anaelea nao, akiwaangalia.

182 Muda si muda mwajua, mmoja wa hawa tai wadogo yuko mgongoni mwake, anapapatika kwa nguvu awezavyo, anayefuata ameinama kifudifudi, anapapatika kwa nguvu awezavyo, lakini mama anawaangalia. Hawajali, wana yubile ya Kipentekoste wakipapatika tu, hawajali. Kama wakivurugika, wakikosa usawa, wanatumainia nguvu kuu, nguvu zinazotosheleza kwa yote za mama yao. Na kama mmoja wa hao jamaa wadogo akivurugika, na kuanza kufingirika upesi kupita kiasi, ama chochote kile, atashuka mbio papo hapo chini yake, na kumwinua, na kumrudisha kwenye neema tena. Amina. Utukufu!

183 Naam, bwana. Usiogope wakati Yeye amekupeleka juu katika nyanja hizi ambazo hata huzielewi, hata hivyo

imeandikwa katika Neno Lake kwa sababu unaangalia kupitia mabawa Yake, Yeye aliahidi jambo hilo, papapatika tu.

184 Jamani, ninaweza kuwasikia wakipaza sauti, "Haleluya! Utukufu kwa Mungu! Mungu asifiwe! Ninaendeleaje? Sijali, bali nina wakati mzuri tu. Utukufu kwa Mungu! Mungu asifiwe! Haleluya!"

Ndipo maskini mama kuku chini ardhini anaangalia juu pale na kusema, "*Chwi*, *chwi*, *chwi, chwi*! Ulokole mtupu!"

185 Hata hajui jambo la kwanza, hajapanda juu kuliko kwenye nguzo ya kitalu. Na mara nyingi dhehebu huvunja mabawa yake kusudi asiweze kupanda juu hivyo.

186 Labda afadhali ninyamaze. Lakini loo, ndugu, ninajua ninalozungumzia. Naam, bwana. Hao kuku hawajui lolote kuhusu mambo ya mbinguni, hawajawahi kuwa huko juu.

187 Wakati fulani uliopita, jamaa fulani alikuwa akihubiri juu ya uponyaji wa Kiungu, sitasema alikuwa ni nani, na mara—mara alipoondoka, kulikuwa na jamaa mwingine aliyekuja pale, na kusema, "Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu. Huyo mhubiri ana kichaa."

188 Kulikuwako na maskini mvulana wa mashambani ameketi kule nyuma, amevaa koti la ovaroli, nywele zimening'inia chini, na kinywa chake, jino moja limetokeza, akaja akitembea humo jengoni namna *hiyo*, kisha akasimama na kumtazama, akainama, akachukua tofaa, akaanza kulimenya *hivi*.

Mhubiri, ama, mtoa mjadala akasema, "Unataka nini, utomvu?"

Akasema, "Ninataka kukuuliza swali." Akaendelea tu kumenya.

Kasema, "Vema, unataka nini?" Akaendelea tu kumenya hilo tofaa. Kasema, "Nena, la sivyo itanibidi, nitakutoa humu."

189 Kasema, "Ninataka kukuuliza swali." Akaendelea kuchonga lile tofaa, mwajua, akaondoa maganda, akalikata, akatoa kokwa, akaweka kipande kimoja kinywani mwake, akaanza kukitafuna namna *hiyo*.

Kasema, "Unataka nini?"

Kasema, "Ninataka kukuuliza swali." Kasema, "Tofaa hili ni tamu au chungu?"

Akasema, "Sijui, silili."

Kasema, "Hivyo ndivyo tu nilivyofikiri."

190 Unajuaje chochote kuhusu Roho Mtakatifu wakati hujapata kumwonja? Hakika, hujawahi kumla, hujawahi kumjaribu. Mjaribu siku moja, ni Asali mwambani. Haleluya! Ni Nguvu za Mungu ziletazo wokovu, u—ule ufufuo wa Yesu Kristo, ni Chakula cha tai, Neno la Mungu, Biblia ya Mungu, Mungu alisema hivyo, hilo latosha milele. "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa

ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Hiyo ndiyo ahadi Yake, Naye hutimiza ahadi Yake. Amina.

191 Maskini tai huyu anapapatika tu, mwajua, wana yubile ya Kipentekoste, wakipaza tu sauti, na kurukaruka. Wa—wana . . . Wanaamini. Kama mama aliwapeleka kule juu, mama anaweza kuwashughulikia.

192 Kama Mungu aliniambia nimwamini, nitamtumaini tu, sijali nitavurugika namna gani, Yeye atanisaidia, kwa namna fulani, sijui. Lakini jambo pekee nijualo, ninataka kupigapiga mabawa yangu, imani yote niliyo nayo katika Agano Jipya na la Kale, loo, jamani, kupapatika huku na huko. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Niendelee tu kupapatika na kuruka.

193 *Kwa njia moja au nyingine*, kama akituma Upepo wa Nguvu Unaoenda kasi, Yeye hutupilia mbali manyoya yote yaliyolegea. Unaweza kulistahimili, la sivyo Yeye asingekupeleka huko juu, weka tu tumaini lako Kwake wakati mmoja, uone atakalofanya, huo ndio mruko wako wa peke yako. Loo, jamani! Najisikia vizuri sana. Nawe je? Loo, jamani!

194 Wakati wa kutaharikisha kiota, kanisa la Kipentekoste linahitaji wakati wa kutaharikisha kiota, linahitaji uamsho wa mtindo wa kale. Kama alivyonena juu ya Yakobo, yeye alikuwa mboni ya jicho Lake, alifanya makosa, bali alimpata nyikani, Naye, kama tai akitaharikisha kiota chake, alimbeba Yakobo juu ya mbawa Zake. Amina.

195 Kanisa limekosa, sote tumefanya makosa, bali sisi ni mboni ya jicho Lake. Yuko tayari kukitaharikisha kiota usiku wa leo, amtume Roho Mtakatifu ndani na kuyang'oa manyoya yote, na kufanya uamsho hapa katika Bonde hili la Yakima utakaolionya taifa hili. Atafanya hivyo. "Kama tai ataharikishavyo kiota chake, na kupapatika juu ya makinda wake, na kuwapeleka juu kwenye mbawa zake, na kuwainua hewani," Yeye alisema, "vivyo hivyo na Yeye alimfanya Yakobo. Nao urithi wa Bwana ni watu Wake." Amina. Jambo ndilo hilo. Urithi wa Mungu ni watu Wake.

196 Alimwambia Musa, akasema, "Mimi ndimi Urithi wako."

197 Hivi majuzi, nilikuwa nimesimama karibu na . . . Hili ni sawa. Nilikuwa nikipitia karibu na Ndugu Tommy Osborn, huyo ndugu mzuri, Mkristo, Tommy Osborn. Aliletwa kwenye huduma yake kule usiku huo wakati yule mwendawazimu alipotimua mbio jukwaani apate kuniua huko Portland. Halafu basi, amesafiri kwenda ng'ambo, naye amefanya ninii . . . Yeye ni—yeye ni mtu mtakatifu wa Mungu. Niliangalia kwenye jengo lake kubwa, akanipitisha pale, jinsi lilivyokuwa la kupendeza!

198 Ndipo huyu hapa akaja ndugu yetu mpendwa, Oral Roberts, mmoja wa watu wazuri sana, na watu wema sana, naye Mungu amemtumainia mali nyingi, na kila kitu. Na hapo nikaenda kwenye jengo lake, nami nikapitia pale, na kuona vitu hivyo

vyote vimejengwa katika mfano wa utatu. Hakuna kioo ubavuni, yote ni marumaru kutoka ng'ambo, na—na dari ni alumini, nyaya zote za alumini zilikuwa karibu karibu, mashine mia tano ama kitu fulani mle ndani, kama tu mstari wa mkutano, zikipita, na barua, na kadhalika. Nikawaza, "Loo, jamani!"

199 Nikatoka nje, nami nikamwambia Ndugu Fisher, ambaye nilifanya umishenari pamoja naye huko Afrika, alikuwa akinipitisha . . . Nami nikaingia kwenye ki—kioo na kuona hiyo mikono mikubwa mizuri ikinyoshwa chini, kama mikono ya Mungu, na wenye dhambi wakimwendea, moyo wangu uliruka tu kwa furaha. Nikawazia, "Ee Mungu, jinsi ninavyokushukuru kwa ajili ya Oral Roberts! Jinsi ninavyokushukuru kwa ajili ya maskini mvulana mmoja wa Kipentekoste, aliyezaliwa kwenye mtumbwi huko ng'ambo, angeweza kupanda kuwa muhimu hivyo!" Nikasema, "Jinsi ninavyokushukuru, Mungu!"

200 Nami nikasimama nje, nikabaki peke yangu na kutembea pande zote na kuingia kwenye gari langu, ndipo kitu fulani kikaniambia, ilikuwa ni Shetani, akasema, "Lakini vipi kukuhusu wewe? Huduma ya Oral ilitokana na yako, vivyo hivyo na ya Tommy Osborn, nawe huyu hapa. Ziko wapi mashine zako za IBM?"

201 Maskini sehemu ndogo mwishoni mwa trela ambayo Ndugu Leo huniruhusu kuwa na ofisi ndani yake, simu imewekwa mle ndani, na taipureta ndogo ya mtumba. "Vipi kuhusu hilo?"

Nikasema, "Loo, hakika ningechukia wao kuja kuona hiyo."

Shetani anasema, "Unaona, Yeye haninii, hawezi kukutumainia."

Nikasema, "Nadhani hiyo ni kweli." Mnaona? "Hao ndugu wote walio na ninii yote . . . Nadhani, Yeye hawezi kabisa kunitumainia, hakuna lingine."

202 Nilikuwa nimesimama pale nikiangalia pale, nami nikahuzunika sana, nikawazia, "Ee Mungu, kadiri nilivyojaribu sana na kadhalika," ndipo nikasema basi, "angalia yale Wewe umefanya . . . "

203 Papo hapo nikasikia Sauti, ikasema, "Lakini Mimi ndiye Urithi wako."

Nikasema . . . Niliwaza:

> Ee Mungu, hema ama kibanda, kwa nini nijali?
> Wananijengea ikulu kule ngambo!
> Ya marijani na almasi, na fedha na dhahabu,
> Makasha yake yamejaa, Ana utajiri usioelezeka.
>
> Mimi ni mtoto, tai, wa Mfalme!
> Mtoto wa Mfalme!
> Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
> Mimi ni mtoto wa Mfalme!

Loo, jamani!

204 Papatika tu basi, endelea tu kama unapanda juu, ama uko chini, ama chochote unachofanya, Mama amesimama moja kwa moja pale nje akipaa juu, moja kwa moja huku, "Jicho lake liko kwenye shorewanda, nami ninajua Yeye huniangalia," ndani na nje ya Kanisa Lake, kuona kama ukitoka kwenye mvurugiko, jambo fulani litatukia, yale—yale Mabawa makubwa, Neno la Mungu, yatakurudisha moja kwa moja juu.

Mtu fulani alisema, "Huo ni moto wa nyika."

205 Afadhali niwe na moto mdogo wa nyika, kuliko kutokuwa na moto hata kidogo, mwajua, hivyo. Vema. Tunaweza kuchukua hayo Mabawa makubwa, na kuyarudisha upande wa kulia. Hiyo ni kweli, ndugu? Kama wakienda nje kidogo ya utaratibu, mbona, tutawashika tu kwenye Ubawa, mnaona, jinsi ilivyo hasa, na kuwarudisha juu katika neema tena. Ukiwaacha tu wapapatike, naam, bwana, acha tu waendelee, wapaze sauti, wamsifu Bwana, na kupiga makelele ya haleluya, wacheze katika roho, chochote wanachotaka kufanya, wakitoka nje ya utaratibu, tuna kitu fulani hapa, Mabawa.

206 Mungu kamwe hatakuacha uanguke kama wewe ni tai, Yeye atakuinua juu tena. Sasa, kama wewe ni koho, unaanguka, kwa vyovyote vile, kwa hiyo utajibwaga tu ardhini. Lakini kama wewe ni tai halisi, utalisikiliza Neno la Mungu. Amina. Utajua hilo ni Ubawa wa Mama ukikurudisha kwenye neema tena. Amina.

207 Kasema, si muda mrefu uliopita nilisikia hadithi fulani, iliyosema mkulima alikuwa akitaka kumwatamisha kuku. Na sijui ni mayai mangapi yanayohitajika kwa kuatamia huku nje, huko chini kusini, mahali ninapotoka, inahitaji mayai kumi na matano kuatamisha. Hilo ni jambo lile lile hapa?

208 Kwa hiyo, maskini mkulima huyu alikuwa na mayai kumi na manne tu, naye akachukua yai la tai na kuliweka chini ya kuku. Angalieni alipata mazao ya aina gani. Hivyo karibu ndivyo ilivyo, karibu moja kutoka kwenye uatamishi mmoja, karibu tu jinsi unavyolipata, hiyo ni kweli, yapata tai mmoja kutoka kwenye uatamishi mmoja.

209 Kwa hiyo maskini yule kuku akayaatamia mayai haya, na hatimaye wakati yote yalipoanguliwa, kama maskini huyo tai hakuwa bata mwenye sura mbaya, katika kundi hilo la kuku! Vema, alikuwa ndiye kitu cha kuchekesha kuliko vyote walichopata kuona.

210 Na hivyo ndivyo baadhi yenu mlivyofanya mlipoanguliwa kweli, miongoni mwa kundi kubwa la kawaida, na baridi, na kadhalika, na lundo la kanuni za imani, tunasema, "Baba yetu, uliye Mbinguni, *Jina* Lako litukuzwe. Salamu, Mariamu, umebarikiwa," na namna hii nyingine yote ya mambo. "Nasi tunaamini katika—katika mambo haya mengine yote," mwajua,

kuhusu, "kwamba tunaamini katika kanisa takatifu la Katoliki, ninii . . . Loo, hii Kanuni ya imani ya Mitume."

211 Laiti mtu fulani angenionyesha Kanuni ya imani ya Mitume katika Biblia. Hmm! Hiyo si Kanuni ya imani ya Mitume. Kama walikuwa na kanuni yoyote ya imani, ilikuwa, "Tubuni!" Hivyo ndivyo Petro alivyowaambia kwenye Siku ya Pentekoste, kasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtampokea Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa watu wote walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

212 Hiyo ndiyo Kanuni ya imani ya Mitume. Hivyo ndivyo ilivyokuwa, si hata moja ya haya, "Ninaamini katika Kanisa Takatifu la Katoliki ya Kirumi, ninaamini katika ushirika wa watakatifu." Mtu yeyote anayeamini ushirika wa watakatifu anakiri ya kwamba wao ni waabudu mizimu. Hiyo ni kweli.

213 "Kuna Mpatanishi mmoja tu kati ya Mungu na mwanadamu, huyo ni Mwanadamu Kristo Yesu." Siamini katika ushirika wowote wa watakatifu, watakatifu wameondoka. Ibrahimu alisema ya kwamba alikuwa ni . . . Yesu alisema ya kwamba alikuwa katika kifua cha Ibrahimu, na kusema asingeweza kuja hapa ama kwenda kule, hizi zote mbili, kwa hiyo hilo latosha, kuna ghuba kati yao ambayo hawawezi kuvuka huku na huko. Wala hakuna ushirika wa watakatifu. Hiyo ni kweli. Ushirika pekee tulio nao ni kupitia kwa Yesu Kristo, huyo ndiye Mpatanishi wetu.

214 Biblia ilisema, "Hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na mwanadamu, ila Mwanadamu Kristo Yesu." Hiyo ni kweli kabisa. "Juu ya Kristo Mwamba imara, ninasimama; sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao."

215 Maskini tai huyu, mama, baada ya kumtoa kwenye kiota, mwajua, kwa namna fulani alimfuata nyuma. Unakumbuka jinsi ulivyoonekana kuwa pabaya? "Jamani, jamani," kasema, "hili halionekani sawa." Katembea kwenye ua huo wa kale wenye vumbi, na—na ambapo ng'ombe wametembea, na farasi, na mavumbi hayo ya kale yakiruka juu, "Hmm, ni uvundo jinsi gani!" Kasema, "Hili halionekani sawa." Akaangalia juu namna *hiyo*, na kusema, "Aisee, vipi kuhusu *kule* juu?

216 Ndipo maskini yule kuku akasema, "*Chwi*, *chwi*, *chwi*, *chwi*, *chwi*, *chwi*! Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama kuruka juu hewani, hilo haliwezekani."

217 Kamwe halikumkalia sawa, mwajua, lilininii tu, halikukidhi sayansi yake ya mapishi. Alijua kuna kitu bora zaidi huko juu mahali fulani, kwa hiyo akaendelea kutembea ameinua kichwa chake.

218 Naye akasema, "Watoto, msimsikilize, yeye ni mmoja wa hao jamaa wa kiajabuajabu," mnaona. Hivyo ndivyo alivyo tai

wakati kwa namna fulani yuko mahali pasipofaa miongoni mwa kuku. Mnaona? Kwa hiyo, anaenda kwenye lundo kubwa la samadi na anaanza kuchakura, akasema, "*Chwi*, *chwi*, *chwi*, *chwi!* Tutakuwa na—tuta—tutakuwa na maskini chakula cha jioni hapa usiku wa leo, hatuna budi kumlipa mchungaji. Hatuna budi kuwa na namna fulani ya mauzo kulipa . . . "

219 Loo, inapofikia mahali kama hapo, kanisa linapaswa kufunga milango yake. Toeni zaka zenu naye mchungaji atalipwa.

220 "Tutakuwa na mchezo wa karata, tutakuwa na mambo haya mengine yote hapa."

221 Maskini huyo tai akaanza, na kusema, "Whiu! Nisingeweza kuvumilia hilo. Jamani! Hmm! Hmm! Jamani!" Akaendelea kuangalia juu, kuangalia juu.

222 Na baada ya kitambo kidogo, maskini mama yake alikuwa akimtafuta, huyu hapa anakuja, akashuka chini kwa kasi, akamwona. Loo, nina furaha sana! Loo, jamani! Akapaza sauti, "Mpenzi, wewe si kuku, wewe ni wangu!"

223 Loo, ninakumbuka wakati niliposikia juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa mara ya kwanza, Yeye alipiga mayowe moyoni mwangu, "Ni kwa ajili yako, nilikuita. Loo, wewe si kuku, wewe ni Wangu."

224 Loo, aliposikia kilio hicho! Alisema nini alipopitia hapo tena, alisema, si, "*Chwi*, *chwi*, *chwi!*" Alisema, "Utukufu! Haleluya! Bwana asifiwe!"

225 Hilo linasikika zuri kwake. Amina. Hilo ndilo aliloenda . . . Hilo ndilo alilozaliwa kwa ajili yake, hiyo ndiyo sababu jina lake liliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Waliposikia hayo, ni kama tu asali juu ya mwamba kwa dubu, atairamba usiku kucha. Mnaona? Anakuja, anajua ya kwamba kuna kitu fulani, "Wewe ni wangu, Mpenzi. Wewe si kuku, wewe ni tai."

"Loo, hivyo ndivyo ilivyo, Mama? Angalia hayo mabawa makubwa."

"Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. MIMI NIKO AMBAYE NIKO."

"Amina. Hilo linasikika zuri. Naam! Nifanye nini, Mama?" Amina.

"Ruka tu juu kadiri uwezavyo kuruka na uanze kupigapiga mabawa, nitakupata." Amina. Haleluya!

Akafanya mruko mmoja na kupapatika mara nne ama tano, naye akagonga moja kwa moja juu ya nguzo, moja kwa moja katikati ya madhehebu.

Akarudi tena, akasema, “Mpenzi, huna budi kufanya vizuri zaidi ya hivyo, la sivyo hata siwezi kukuchukua.”

226 Tunachohitaji leo ni wakati wa kukitaharikisha kiota, tunachohitaji leo ni nguvu za Roho Mtakatifu, tunachohitaji leo ni Chakula cha tai, kuhubiri ya kwamba Yesu Kristo angali anaponya, Yeye ni yule yule, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.”

227 Hivi hamna furaha kujua, usiku wa leo, ya kwamba Yehova ana mbawa Zake kubwa hapa, akipeperusha Roho Wake huku na huko? Malaika wa Bwana akipigwa picha, Nguzo ile ile ya Moto iliyokuwa nyikani katika Agano Jipya sasa katika siku za mwisho, jana, leo, na hata milele, watu wakiponywa kujazwa na Roho Mtakatifu, wakinena kwa lugha, tafsiri, nguvu za Mungu zikija, Bwana akikaribia, Mungu akilileta Kanisa Lake pamoja, hivi hamna furaha kuwa katika kitu kama hicho? Mna furaha? Amina. Whiu!

228 Jamani, sijui kama ninaweza kwenda muda mrefu zaidi au la, hili linaonekana kama, karibu kuanza safari sasa hivi. Hili linasikika zuri kwangu, kujua kwamba ni kweli, si hadithi ya Baba Krismasi, ni kweli ya Mungu aliye hai. Mnaamini hilo? Naam, kwa moyo wako wote? Unaamini tunahitaji wakati wa kukitaharikisha kiota? Je, mnahitaji—mnahitaji Roho Mtakatifu tena? Mnaamini tunahitaji kumwagwa upya kwa Roho? Mnaamini Kanisa linahitaji kubatizwa upya tena? Unaamini kwa moyo wako wote? Hebu tuanze jambo fulani sasa hivi, sivyo? Mko tayari kuingia chini ya Upepo? Mko tayari kufanya hivyo? Mnaamini hilo?

229 Hebu na tusimame kwa miguu yetu. Ni watu wangapi hapa wasio na Roho Mtakatifu? Ni watu wangapi wasio na Roho Mtakatifu? Njoni hapa kwa dakika moja, shukeni mtoke kwenye roshani hiyo. Huu ni wakati wa kutaharikisha kiota. Hebu tung’oe maskini manyoya haya yaliyolegea. Hatuwezi kuponya wala kuwa na ibada halisi ya uponyaji mpaka tutakapoyaweka haya manyoya moja kwa moja. Mungu kamwe hatatupeleka kule juu na kutuangusha mpaka tutakapoyaondoa manyoya haya kwetu.

230 Njoo sasa, kila mtu anayetaka kuja chini ya nguvu za Roho, njoni hapa juu, kwa dakika moja tu, na usimame karibu na madhabahu hii. Ninaamini Mungu atamwaga Roho Mtakatifu papa hapa usiku wa leo, na kukitikisa kitu hiki, na kuondoa manyoya yote hapa, na kuwachukua tai Wake juu ya mbawa namna *hiyo* na kutupeleka huko nje kwa ajili ya uamsho.

231 Ninataka kuona uamsho ukiachwa hapa. Ninataka kuona kila moja ya makanisa haya yakiwaka moto, nguvu za Mungu zikishuka. Unaihitaji. . .Shuka utoke kwenye roshani, ndugu, usiliahirishe tena. Sikiliza, kama wewe ni mwenye dhambi, njoo,

pia, njoo moja kwa moja, wewe usiye na Roho Mtakatifu, ninyi msio na toba, songeni moja kwa moja madhabahuni.

"Loo," unasema, "ni mbali sana huko chini."

232 Ukikosa kuipata, siku moja kuzimuni itakuwa ni mbali sana kurudi kutubu tena. Ni karibu sana hapa kuliko ingekuwa kutoka kuzimuni. Njoni. Wote wasio na vita, hakika hupitia njia ya kuzimu. Njoni, jambo ndilo hilo. Njoni, enyi tai. Mmemsikia akipiga makelele usiku wa leo? Je, mumeuhisi Uwepo Wake? Je, mumeuhisi huo Upepo ukisema, "Huu ndio, huu hapa, ndio huu."

233 Hii ndiyo ile ile waliyokuwa nayo kwenye Siku ya Pentekoste, hizi ndizo nguvu halisi za Mungu, hizi hapa. Ninangojea, wanatoka kwenye roshani, baadhi yao wakishuka.

234 *Kuna Chemchemi Iliyojaa Damu*, tafadhali, ndugu kwenye kinanda. Hebu tuuimbe sasa, tunapongojea tai wote wakusanyike. Loo! Bwana abarikiwe!

Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "*Hili* ni *Lile*." Kama *Hili* si *Lile*, nitashika tu *Hili* mpaka *Lile* litakapokuja. Amina. Njoni!

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye ninii ya Imanueli . . .

235 Wewe unayetaka kumfanyia Mungu kazi, kama wewe ni mke wa nyumbani, Yeye atakupa karama ya kunena kwa lugha, Atakupa karama ya unabii, atakufanyia jambo fulani. Hivi hutakuja? Yaondoe manyoya yaliyolegea sasa.

. . . ninii yao yote ya hatia . . .

236 Hivi hutakuja? Njoo kutoka kwenye roshani, rafiki mwenye dhambi, shuka chini, njoo huku. Ninyi nyote ambao ndio kwanza mmemkubali Kristo kama Mwokozi binafsi, ingawa hamjajazwa na Roho Mtakatifu, hivi hamtakuja madhabahuni? Mungu akubariki, mama.

Wanapoteza madoa yao yote ya hatia; (Papa hapa, mama, moja kwa moja ndani hivi.)
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya gharika hiyo,
Hupoteza ninii yao yote ya hatia . . .

237 Sikilizeni, marafiki, hii ndiyo njia pekee kwenu kumpendeza Mungu, ni kutii. "Wale wamjiao Mungu hawana budi kumwamini."

238 Sasa angalieni, baadhi yenu ninyi Methodisti, Baptisti, Presbiteri, ama wengine ambao hawajampokea Roho Mtakatifu bado, Mungu angeniruhusuje kufanya mambo haya anayofanya hapa usiku? Yeye angenitumaje hudumani, mara saba kote ulimwenguni? Angefanyaje jambo hilo, kuacha mamilioni ya watu wavutwe, kama sikuwa na wazo fulani la ukweli?

Angeniruhusuje kufanya mambo haya, ishara ambazo alisema angezituma katika siku za mwisho? Nasi hata hatujawahi kuziona wala kusoma habari zake katika historia hapo kabla, tangu siku za Bwana wetu. Kwa nini aniruhusu kuleta Ujumbe kama huu, kama nimekosea? Yeye—Yeye kamwe hataubariki uongo. Lakini Yeye huniruhusu kuuleta, kwa sababu nimehubiri hii ni kweli; hii ndiyo njia.

239 Basi sikiliza, ewe rafiki Mkatoliki, hivi ulijua bikira Mariamu ilimbidi kupanda juu na kumpokea Roho Mtakatifu, na kuyumbayumba kana kwamba alikuwa amelewa, kabla Mungu hajamruhusu kuingia Mbinguni? Utafikaje huko na chochote pungufu ya huo? Kanisa lako, kanuni yako ya imani, chochote kile, kama ni kanuni ya imani ya Kipentekoste, kama ni kanuni ya imani ya Kibaptisti, ama kanuni ya imani ya Kimethodisti, chochote kile, kamwe hutaingia kwa chochote pungufu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli kabisa.

Kwa hiyo, ulisema, "Inaonekana ni ya kigeni sana."

240 Naam bwana. Ni kitu gani kinachowafanya watu hawa kutenda hivyo? Ni kwa sababu wamezaliwa kutoka Juu. Roho yao ni ya Ufalme mwingine, Ufalme wao uko juu. Yesu alisema, "Kama ulimwengu huu ungekuwa Ufalme Wangu, watu Wangu wangeupigania, bali Ufalme Wangu uko huko juu." Hiyo ni kweli.

241 Hivi hamtakuja? Hebu tuimbe mara nyingine tena ili niwe na hakika. Nimeomba tu siku nzima ya kwamba Mungu angepajaza mahali hapa na kupatikisa kuliko hapo awali, mnaona.

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuona,
Ile . . .

242 Unaamini sasa, kwa moyo wako wote? Shuka utoke hapo. Hivi hutashuka? Tafadhali, rafiki, ninakushawishi katika Jina la Kristo.

. . . hapo naomba, nijapokuwa mwovu kama yeye,

Wewe ni mwovu kama yeye kama ukimkana.

. . . dhambi zangu zote,

Njoo moja kwa moja, hiyo ni kweli.

Nioshwe dhambi zangu zote,
Nioshwe dhambi zangu zote;
Na hapo naomba, ingawa ni mwovu . . .

243 Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, hebu na tusimame kwa muda kidogo tu. Sasa, kama mnanichukua kama mtumishi Wake, kama kweli mnathamini hilo, ninaweza kuwasaidia. Sasa, ninyi nyote hapa mnaomtafuta Roho Mtakatifu wa Mungu, inueni mikono yenu. Mnaona njaa, Yesu alisema, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, hao watashibishwa."

244 Sasa, kuna kundi la watu hapa nje ninalotaka kulishughulikia kabla mimi, hatujaenda chumbani mle. Lakini ninawatakeni ninyi watu hapa, mnaomtafuta Roho Mtakatifu kumfuata mmoja wa wahudumu hawa. Nani...? Yupi—yupi kati ya...? Ndugu huyu papa hapa, ongoza, ingia chumbani, hapa kwa dakika moja tu. Hapa, ingia hivi: "Bwana, usiponipa Roho Mtakatifu, utakaporudi duniani nitakuwa nimelala papa hapa." Unaona?

245 Kamwe usi—usiuchezee. Ukifanya hivyo, kamwe hutafika popote, huna budi kulidhamiria. Huna budi kuja kwa Mungu ukiamini ya kwamba utapata kile Yeye...Kwa nini—kwa nini Yeye akasema hivyo...?

246 Nilisema muda mfupi uliopita hao watu wasingeweza kumtoa huyo pepo mchafu, walisema, "Mbona, tusingeweza kufanya hivyo?"

Akasema, "Kwa sababu ya kutokuamini kwenu."

247 Si kama hawakuwa na mamlaka ya kufanya hivyo, bali hawakuwa na imani ya kufanya hivyo. Sasa, una nguvu za kumpokea Roho Mtakatifu, una Roho Mtakatifu juu yako, kwa sababu unaona njaa na kiu, naye Yesu alisema, "Mmebarikiwa, kwa sababu hata mna njaa na kiu." Sasa nisikieni na muamini.

248 Ingieni moja kwa moja mle ndani sasa, wakati nikilishughulikia kundi lingine hapa, nitakuwa huko ndani katika dakika moja tu. Vema. Sasa, mnapochukua mahali penu papa hapa, nendeni moja kwa moja hivi chumbani, kusudi tusiwasumbue hao wengine. Wakati mwingine, watu wakimtafuta Roho Mtakatifu, wanafikiri mtu fulani yuko kule nyuma, "Nilimleta Bw. Jones, naye ameketi kule nyuma." Lakini jipeleke mwenyewe, mahali ambapo kila mtu anakufa pamoja nawe, jambo fulani litatukia. Hiyo ni kweli. Ingia tu moja kwa moja chumbani.

249 Hebu sote, tulio na Roho Mtakatifu, tuseme, "Mungu asifiwe." Angalieni huu msogeo mkuu...Angalieni nguvu hizi kuu za...

250 Sasa, ninyi nyote wafanyakazi wa kibinafsi ingieni moja kwa moja pamoja nao sasa, wafanyakazi wote wa kibinafsi. Baadhi yenu ndugu wahudumu, mkipenda, pia, aingieni mle ili mhakikishe ya kwamba kila kitu kinaendelezwa sawasawa kabisa. Tunawataka wapokee ubatizo halisi wa Roho Mtakatifu. Ingieni moja kwa moja chumbani, ili wakutane nanyi mumu humu ndani, katika dakika moja tu.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
gharika hiyo,
Hupoteza waa lao lote la hatia.
Hupoteza waa lao lote la hatia,

Hupoteza waa lao lote la hatia;
Na . . .

Kuna mwingine angetaka kwenda? Mmoja zaidi?

. . . chini ya gharika hiyo,
Hupoteza waa lao lote la hatia.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Kwa uchaji:

. . . wimbo mzuri, mtamu zaidi,

251 Sasa, kama kuna yeyote hapa ndani, anayejisikia hivyo huku vichwa vyenu vimeinamishwa, macho yenu yamefumbwa, kwamba wewe si Mkristo, wewe si Mkristo, unasema, "Nilipaswa kuingia mle, bali ninataka kumwinulia Mungu mikono yangu, na kusema, "Mungu, nipe ujasiri, usiniache nife katika hali hii."

252 Marafiki, hatuigizi kanisa. Huenda likaonekana la kipekee kwa yale mliyofundishwa katika kanuni zenu mbalimbali za imani na makanisa, lakini hii ni Biblia, hivi ndivyo ilivyokuwa hapo mwanzo, na Mungu hana kikomo wala hawezi kubadilika. Haya ni yale yale, maagizo yanasema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

253 Sasa, kama humjui Yeye kama Mwokozi wako, naomba u—uwe tu muungwana, ama mama wa heshima kutosha kuinua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham, mimi si Mkristo."

254 Mungu akubariki, ewe msichana. Katika roshani upande wa kushoto, kwenye sakafu kuu, kuna mmoja hapa angesema, "Mimi—mimi si Mkristo, Ndugu Branham, mimi . . . " Mungu akubariki, mama. Ni—nina ujasiri kwa mtu ambaye—ambaye ni mwaminifu. Kamwe hutafika mahali popote na Mungu mpaka utakapokuwa mwaminifu. Upande huu? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mwanangu.

255 Juu kwenye roshani mkono wangu wa kulia, inua mkono wako, useme, "Mimi si Mkristo." Mungu akubariki, mama. Mungu awabariki. Naam. "Mimi si Mkristo, lakini kwa kweli nataka kuwa, Ndugu Branham. Naomba ya kwamba Mungu atanipa ujasiri wa kuja, bado. Ama asiponipa, asiniache nife hivi."

256 Hakika, hamtaki kufa hivyo, enyi watoto. Kwa nini wewe . . . Ni kitu gani kilichokufanya uinue mkono wako? Kwa sababu kitu chenyewe kilicho ndani yako, umezaliwa kuwa tai. Hicho ndicho kilichokufanya uinue mkono wako. Sasa, usi—usi—usiache tu maskini hayo manyoya ya pini na kadhalika yakuzuie kuruka Mbinguni. Kwa nini usifanye hivyo usiku wa leo?

257 Baba yetu wa Mbinguni, kuna hao watu saba ama wanane, wengi wa hao, wengi wao ni vijana katika umri wa utineja, kwenye njia panda tu, niliwaona wale wasichana warembo, wenye sura nzuri, vijana wanaume, wakiinua mikono yao,

wana—wana njaa, Bwana. Roki na mambo ya ulimwengu hayawezi kamwe kuridhisha sehemu hiyo katika moyo wa mwanadamu, mpaka Mungu aingie mle, kama kuna mahali popote pale kwa ajili Yake. Kama wakati alipomfanya mtu huyo, alijifanyia Mwenyewe mahali pa kukaa, hakuna kitu kitakachochukua mahali pake.

258 Baba, jalia wajue hilo ndilo jambo kuu kuliko yote lililowahi kuwapata ni wakati imani ilipokuja nafsini mwao kwamba wangekutumikia, walitaka kukutumikia Wewe. Ninawaombea, Baba, hata sasa, wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kwamba hao watu walioinua mikono yao wataingia moja kwa moja kwenye chumba hicho, hao watoto wadogo, Bwana, si chochote ila—ila watoto matineja.

259 Ninaomba, Baba, ya kwamba wote walioinua mikono yao watakuwa na ujasiri, basi maombi yangu na yaende mbele Zako yakabishe mlangoni mara nyingine tena, Baba. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] Tujalie. Labda wataingia, jambo kuu kuliko yote walilopata kufanya.

260 Ninaweza kukumbuka huko nyuma katika siku za mwanzoni za ujana wangu, jinsi ambavyo usiku huo nilikuwa nikiona njaa, nami ni—nikakuhisi ukibisha mlangoni pangu, Bwana, ni—nina furaha sana nilikuruhusu uingie. Sasa mimi ni mtu wa makamu, ninakupenda tu zaidi ya nilivyowahi kukupenda maishani mwangu. Ee Mungu, kamwe usiruhusu chochote kitendeke kwa. . .kama siwezi kukutumikia Wewe, nichukue sasa, jalia niende sasa. Ni furaha jinsi gani, na majaliwa kumtumikia Mungu!

261 Wape hawa vijana, Bwana, wana vita vikali sana, waangalie, angalia walicho nacho, angalia televisheni yao, imeoza na imechafuka, angalia taifa wanalokulia humu, siasa zimeoza kabisa, mpinga-Kristo akiinuka kitini na mamlakani. Ulimwengu, Wamarekani, hawajui mapambano ni nini, hawajui kujinyima, kamwe haikuwalazimu kukosa mlo. Ee Mungu, angalia tu. Mapambo na Hollywood, na hata imekuwa ni dini ya kupokezana makanisani, na Hollywood, iliyokarabatiwa. Hakuna tena mikutano ya maombi usiku kucha ya mtindo wa kale, na kuugua sana, na kuomba, na kuwa na ushirika kwenye mambo ya Mungu, hakuna tena kuomba ukafanikiwa. Mungu, watoto hawa wanahitaji hayo, naomba ya kwamba watayapokea usiku wa leo.

262 Ninafunga macho yangu, Bwana, Nitaamini ya kwamba utamtuma kila mmoja wao moja kwa moja kwenye chumba hicho. Tujalie, Baba. Jalia litendeke, Bwana, naomba litendeke. Nami ninaweza kuwapa mkono kwenye siku ile, na kusema, "Naam, maskini ujumbe mdogo, uliokatikakatika usiku mmoja, *Kama Tai Ataharikishavyo Kiota Chake*."

263 Ulikitaharikisha kiota cha ulimwengu walimoishi, wanachoshwa nacho, Bwana. Wanainua mikono yao, wanaangalia juu, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu!" Jalia wakimbie, Bwana, waingie kwenye furaha za Kimbinguni, ambapo wanaweza kushiriki huko juu pamoja na jamaa mwenzao wa Injili ile ile. Chakula cha Tai jalia wakile. Tujalie, Bwana. Wasiwe kuku wa ardhini ambao mbwa mwitu na hao wasichana, upuuzi huo wa kale wa mbwa mwitu walio nao siku hizi, wa bugi-wugi, na roki, na uwajalie kujua, Bwana, ni kitu tu cha kurarua nafsi zao za thamani zitoke ndani yao, na kuwapeleka kwenye jehanamu ya ibilisi, kufanya migumu mioyo yao, kuivuta kupitia maskini hadithi hizi za sinema, na hadithi za kweli, wakati yote ni uongo, na hadithi za uongo, na zilizobuniwa.

264 Jalia waangalie Mabawa haya makubwa ya Mungu, Agano Jipya na la Kale, waseme, "Hapo nitasimama, papo hapo juu ya ule Mwamba." Tujalie, Bwana. Ninatumaini ya kwamba kila mmoja wao yuko kwenye chumba hicho sasa. Tujalie, naomba, katika Jina la Kristo. Amina.

Hebu na tusimame tu kimya kwa dakika moja.

[Ndugu fulani ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mwingine anafasiri. Unabii unatolewa—Mh.] Utukufu. Haleluya! Utukufu.

265 Mungu asifiwe. Enyi marafiki, hiyo ni kusema, kama ninaelewa Maandiko, hiyo ni Sauti ya Mungu ikijibu katika uthibitisho, Alirejea na hilo. Yeye alisema nini? "Msiasi, ingieni chumbani." Kila mwenye dhambi asiye na Damu ya Kristo, ingia chumbani, rafiki. Kama Biblia haininii . . . Samahani kwa kusema *kama*, tunajua Biblia ni sahihi, hiyo si sauti yangu, hiyo ni Sauti ya Mungu ikinena. Na kwenu ninyi watu mlio wagonjwa, mnasikia aliyosema? Huo ni Ujumbe kwa Kanisa. Mnaona? Huyo ni Roho Mtakatifu.

266 Sasa, hebu na tuimbe, "Msalabani, msalabani ambapo niliiona Nuru kwa mara ya kwanza." Hebu kila mwenye dhambi arudi humu ndani, hivi mtarudi tafadhalini? Songeni hapa nyuma, kama—kama . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

> Msalabani, msalabani ambapo kwanza mimi . . . (Hiyo ni kweli, rudini moja kwa moja nyuma.) . . . Nuru.
> Na mzigo wa moyo wangu ukafingirika . . .

Wengine wenu mnaweza kuketi, mkitaka.

> Hapo ndipo . . . ambapo nilipokea ninii yangu . . . (Wafanyakazi wa kibinafsi harakisheni kwenda chumbani, upesi sana.)
> Sasa, mimi . . .

267 Kila mtu anayetaka kujitolea kama mfanyakazi wa kibinafsi, sogea, wanakutana chumbani mle, ambamo watu wanampokea Roho Mtakatifu.

> Pale Msalabani, pale msalabani ambapo niliiona Nuru kwanza,
> Na mzigo wa moyo wangu ukafingirika, (Ukafingirika!)
> Hapo ndipo kwa imani nilipata kuona,
> Na sasa nina furaha siku nzima!

Hebu tuuvumishe tu, na tumwinulie Mungu mikono yetu.

> . . . ukafingirika . . .

268 Ee Mungu, tunakupenda, Bwana, tunakupenda.

> . . . nikapata kuona,
> Na sasa nina furaha siku nzima!

269 Sasa polepole sana na kwa utamu, na katika tuni mnayoimbia:

> Pale msalabani, pale msalabani ambapo niliiona Nuru kwa mara ya kwanza. (Kwenye kiota, unaona.)
> . . . mzigo wa moyo wangu uliondoka, (Nilipoyaona mabawa Yake mawili makubwa.)
> Hapo ndipo kwa . . . (nilipanda juu yao.) . . . Nikapata kuona,
> Na sasa nina furaha siku nzima!

270 Loo, kamwe siwezi kuuachilia huo. Si ni mtamu? Hivi huuhisi moyoni mwako?

> Na ninii . . .

60-0804 Kama Tai Ataharikishavyo Kiota Chake
Eisenhower High School
Yakima, Washington Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org